# ATHARI ZA FASIHI SIMULIZI KATIKA RIWAYA YA *UTUBORA MKULIMA.*

NA

KENGURU P.J.MAINA

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA

CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

Novemba, 2013

University of NAIROBI Library
0389970 5

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kingine chochote kile, kwa mahitaji ya shahada ya uzamili.

-------------------------------------------------- 15-11-2013

Tarehe

Kenguru P.J.Maina

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

-------------------------------------------------- 15-11-2013

Daktari Evans M.Mbuthia. Tarehe

-------------------------------------------------- 15/11/2013

Daktari Mwangangi Musyoka Tarehe

## TABARUKU

Kazi hii namtabarukia mke wangu kwa kuyavumilia matatizo mengi yaliyotokana na uamuzi huu wa kujitosa katika masomo ya shahada ya uzamili na kwa ushauri wake wa hapa na pale ulionifaa kwa mchakato mzima wa masomo haya.

Pia nawatabarukia watoto wangu wapendwa kwa kuuvumilia upweke wa kuwaondokea na kuhudhuria masomo haya na mama na ndugu na jamaa kwa msaada wao wa kifedha na ushauri ulionifaa sana.

## SHUKRANI

Kwa heshima na taadhima, napenda kluwashukuru wote waliochangia ufanisi wa utafiti huu kwa njia moja au nyingine.Tasnifu hii isingekamilika kama si kwa ushauri, uelekezi na usaidizi na uelekezi wao murua.

Kwanza kongole zangu ni kwa Manani kwa kuniwezesha kuitimiza ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili katika somo nilipendalo la Kiswahili.Shukrani za dhati ni kwa wasimamizi wangu mahiri na wema Dkt.Evans M. Mbuthia na Dkt.Mwangangi Musyoka kwa mawaidha kabambe na mashauri na uelekezi wa kipekee katika kuiandika tasnifu yangu.

Vilevile namshukuru Prof. Mwenda Mbatiah kwa juhudi za kunifungua macho kuhusu uandishi wa tasnifu. Shukrani zangu aidha ni kwa waadhiri wangu wa kupigiwa mfano katika ulimwengu wa wasomi kwa kuninoa nikanoleka,nao ni: Prof. John Habwe, Prof.Mwenda Mbatiah, Prof. Kineene Wa Mutiso, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Evans M Mbuthia, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Amiri Swaleh, Bw. Basilio Mungania na waadhiri wote wa Idara Ya Isimu Na Lugha za Kiafrika kwa ushirikiano na mipangilio mwafaka kuhakikisha kuwa wanafunzi wa idara hii wamepata si bora mafunzo ila mafunzo bora.

Hali kadhalika nawashukuru wenzagu wote kwa ushirikiano bora katika jitihada za kufuzu katika masomo haya, wakiwemo Bw.Modgen Chisia, Benard Ogola, Bi. Grace Mjomba, Bi.Joyce Onyoni, Bw. Sabastian Mswenje, Bi.Ruth Naliaka na wengineo wengi nisioweza kuwataja kwa sababu ya nafasi.Mungu awajalie kwa lolote mfanyalo.

Mwisho nawashukuru waalimu wenzangu tunaofunza nao na marafiki wote waliochangia kwa njia yoyote ile katika masomo yangu ,wote niliowataja na wale ambao sikuweza kuwataja Jalali awamiminie barakasiku maishani.

**MUHTASARI**

Utafiti huu umeshughulikia *athari za fasihi simulizi* katika uandishi wa riwaya ya *Utubora Mkulima*.

Sura ya kwanza ni somo la utafiti,madhumuni,maswali ya utafiti,sababu za kuchagua somo,upeo na mipaka,misingi ya nadharia na yalioandikwa kuhusiana na mada hii na methodolojia.

Sura ya pili imeshughulikia tawasifu ya Shaaban Robert mwandishi wa riwaya ya *Utubora Mkulima,* falsafa yake kuhusu, fedha, dini, ndoa na athari za waandishi wengine katika uandishi wake.

Katika sura ya tatu tumeangazia suala la mwingiliano matini kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi tukizingatia Historia na mazingira, wahusika na tamathali za semi.

Sura ya nne tumeshughulikia suala la usimulizi na sura ya tano ni hitimisho linaloangazia matokeo ya utafiti, mapendekezo kuhusu utafiti wa baadaye. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya vikale.

# YALIYOMO

UKURASA

UNGAMO..........(i)

TABARUKU..........(ii)

SHUKRANI..........(iii -v)

MUHTASARI..........(v)

**SURA YA KWANZA**

1.0 UTANGULIZI .......... 1-2

1.1 TATIZO LINALOTAFITIWA .......... 2-3

1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI .......... 3

1.3 MASWALI YA UTAFITI.......... 3

1.4 SABABU YA KUSHUGHULIKIA TATIZO HILI.......... 4 -5

1.5 UPEO NA MIPAKA .......... 5

1.6 MSINGI WA NADHARIA .......... 6-8

1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO .......... 8-11

1.8 NJIA ZA UTAFITI .......... 11

1.9 KIMALIZIO .......... 11-12

## SURA YA PILI

## MAISHA YA SHAABAN ROBERT

2.0 UTANGULIZI...........................................................................13

2.1 MAISHA YA SHAABAN ROBERT KWA UFUPI................................13-16

2.2 KAZI YA KI NATHARI ZA SHAABAN ROBERT................................16 - 18

2.3 FALSAFA YA SHAABAN ROBERT..........................................18-22

2. 4 KUHUSU FEDHA......................................................................22 - 24

2.5 KUHUSU DINI ..............................................................24-25

2.6 KUHUSU NDOA......................................................................25-26

2.7 ATHARI ZA WAANDISHI WENGINE.......................................26-28

2.2.0 KIMALIZIO...........................................................................28

**SURA YA TATU**

**MTAGUSANO KATI YA FASIHI SIMULIZI NA FASIHI ANDISHI**

3.0. Utangulizi ....................................................................29

3.1 Mwingiliano matini....................................................................29-33

3.2 Historia na mazingira....................................................................33-34

3.3 Wahusika ....................................................................34-39

3.4 Tamathali....................................................................39-40

3.5 Chuku....................................................................41-42

3.6 Nahau....................................................................42-43

3.7 Tashbihi....................................................................43-44

3.8 Kinaya....................................................................45-47

3.9 Taharuki....................................................................47-48

3.10 Sadfa....................................................................48-49

3.11 Majazi....................................................................49

3.12 Ritifaa....................................................................50

3.13 KIMALIZIO....................................................................50-51

**SURA YA NNE**

**USIMULIZI KATIKA RIWAYA YA UTUBORA MKULIMA.**

4.0 Utangulizi....................................................................52-53

4.1 Aina za usimulizi..........................................................53-55

4.2 Nafsi ya kwanza............................................................55-57

4.3 Nafsi ya pili......................................................................57

4.4 Nafsi ya tatu...................................,,,,........................58-61

4.5 Kimalizio ..........................................................................62

**SURA YA TANO**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

5.0 UTANGULIZI.....................................................................63

5.1 MUHTASARI ...............................................................63-65

5.2 HITIMISHO..........................................................................66

5.3 MAPENDEKEZO...................................................................66

MAREJELEO.....................................................................67-68

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Tanzu za mwanzo kabisa katika jamii zote ni zile zinazohusiana moja kwa moja na Fasihi Simulizi, kama vile mashairi, ngano, vitendawili, visaasili, methali, uigizaji na kadhalika. Baadaye baadhi ya tanzu hizi zilijitokeza katika maandishi. Chimbuko la riwaya ya Kiswahili ni ngano za kisimulizi.

Zaja J.O (1986), Katika tasnifu yake ya uzamifu alieleza kuwa fasihi andishi kulingana na wanahistoria wa fasihi ya Kiswahili, ilichipuka kwa kutumia hati za Kiarabu na ilijikita katika utanzu wa ushairi. Maingiliano haya kati ya Waswahili na Waarabu yalibadilisha mfumo wa awali wa fasihi kusimuliwa na kuchukua mfumo wa ushairi na kuchangia katika kupanua kiwango cha fasihi iliyokuwepo kabla ya kuja kwa wageni hawa.

Maoni haya yalitufaa katika utafiti huu kwani yanathibitisha kuwa ushairi ambao ulikuwa na mashiko katika Afrika Mashariki kuliko tanzu zingine, una athari katika kazi za kibunilizi za riwaya hasa riwaya ya *Utubora Mkulima*. Shaaban Robert katika riwaya hii ameyatumia na hivyo kudhihirisha athari hizi.

Vilevile baada ya kuingia kwa wageni wa Kimagharibi hasa wamishenari, ngano kadha wa kadha zilitafsiriwa na zikawa ndio msingi wa riwaya za kisasa. Baada ya mwaka wa 1940 na kuendelea hadi miaka ya sitini, riwaya nyingi zilifuata mkondo wa ngano za fasihi simulizi zilozokuwa na mianzo kama vile "Paukwa Pakawa..." "Hapo zamani za kale Paliondokea ..." Kimaudhui, nyingi zilikuwa na mambo ya mila na tabia kama njia ya kufunza maadili.

Riwaya za awali nyingi zilikuwa na wahusika binadamu na wanyama. Sababu kuu ni kuwa, fasihi simulizi ilikuwa njia ya kuelewa na kutawala mazingira au matukio ya mara kwa mara katika jamii. Waandishi wa kazi za kubuni walichukua malighafi yao kutoka kwa mazingira yao. Mawazo haya yanaungwa mkono na Mwandawiro J.D.M (1984), katika tasnifu yake anaposema kuwa "Huko Unguja kulikuwa na makabwela kati ya wenye ardhi na wasio na ardhi,matajiri na masikini,tabaka hizi zilijitokeza katika fasihi simulizi.

Mlacha S.A. K na Madumulla.J.S (1986), pia walisema kuwa, katika kuzungumzia historia ya riwaya ya Kiswahili ni muhimu kuihusisha sanaa na fasihi simulizi. Uhusiano huu sio wa kimuundo, ingawa muundo wa masimulizi ulichangia kwa kiasi kikubwa katika riwaya nyingi za mwanzo.

Mawazo haya ya Mlacha na Madumulla kuhusu uhusiano uliopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi kwa kiasi kikubwa unathibitisha kuwa fasihi simulizi ambayo ni ya awali kuliko fasihi andishi ina athari kubwa katika fasihi andishi ambayo ilitokea baadaye. Matumizi ya methali, vitendawili, mashairi na kadhalika katika riwaya nzima ya *Utubora Mkulima* vinaakisi ukweli kuwa athari za fasihi simulizi zingali hai katika jamii na kudhihirika ndani ya riwaya za Kiswahili. Athari hizi ndiyo jira ya tatizo letu la utafiti.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Utafiti wetu unanuia kutafiti kuhusu athari za fasihi simulizi katika riwaya ya *Utubora Mkulima* kwani tatizo hili halijashughulikiwa na watafiti wa awali.

Katika utafiti wetu tunatarajia kubainisha vipengele kama vile hadithi, ngano, vitendawili nyimbo na kadhalika jinsi vinavyokamilisha riwaya hii ya *Utubora Mkulima*.

Tigiti. S na S.Kiango, (1978), vilevile walisema" Imani iliyopo ni kwamba, fasihi simulizi ni ghala ya asilimali na amali kubwa ya uafrika wetu na kwamba waandishi kama vile Shaaban Robert na wengine wasingefaulu kujitokeza kama waandishi wa vitabu kama si kutokana na hadithi za akina bibi.Hii ni dhahiri kuwa, kazi za kubunii za Shaaban ikiwemo riwaya ya *Utubora Mkulima* zina athari ya fasihi simulizi.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti huu una madhumuni yafuatayo:

1. Kubainisha vipengele mbalimbali vya Fasihi Simulizi alivyotumia Shaaban Robert katika riwaya ya *Utubora Mkulima*.
2. Kutathimini ufanisi wa Fasihi Simulizi katika kuikuza na kuipa mashiko riwaya ya *Utubora M*kulim*a*.
3. Kulinganisha maudhui na mtindo wa Fasihi Simulizi katika riwaya ya *Utubora Mulima*

## 1.3 MASWALI YA UTAFITI

1. Je, ni vipengele vipi vya Fasihi Simulizi vilivyotumiwa na Shaaban Robert katika riwaya ya *Utubora Mkulima*?
2. Je, fasihi simulizi ina mchango wowote katika kuikuza na kuipa mashiko riwaya ya *Utubora Mkulima?*
3. Je, riwaya ya *Utubora Mkulima* ina uhusiano wowote wa kimuundo na kimaudhui na Fasuhi Simulizi?

## 1.4 SABABU YA KUSHUGHULIKIA TATIZO HILI

Tumechagua kutafiti kuhusu athari za Fasihi Simulizi katika riwaya ya *Utubora Mkulima* kwa sababu athari za fasihi simulizi hazielekei kupewa uzito unaostahili na waandishi wengi wa kinathari ambao wameegemea katika uandishi wa utanzu wa riwaya.

Sababu nyingine ni kuwa mafunzo haya ya fasihi simulizi yalikuwa na mashiko katika jamii za awali na yalikuza maadili miongoni mwa wanajamii, hali ambayo inaonekana kufifia katika jamii za kisasa, kisa na maana mafunzo haya yaliotokana na fasihi simulizi yamegubikwa na fasihi andishi inayoenea kwa kasi sana miongoni mwa jamii.

Kichocheo kingine ni kuwa wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili wanamsawiri Shaaban Robert kama 'daraja' au kiunzi kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Hivyo basi imekuwa ni muhimu kuweka wazi athari hizi za fasihi simulizi katika fasihi andishi tukijikita katika riwaya ya *Utubora Mkulima* ili kubainisha kuwa riwaya hii vilevile imesheheni athari za Fasihi Simulizi kwani inaandikwa katika kipindi ambacho fasihi simulizi ilikuwa imekita mizizi katika jamii za Kiafrika

Kwa mujibu wa Ogechi O.N. na wenzake, (2008:94), fasihi ya kisasa ya Kiswahili ilianzishwa mnamo miaka ya hamsini na sitini kwa vumbuzi za Shaaban Robert na wafuasi wake haswa katika eneo la nathari. Maandiko yao yalilenga zaidi madhumuni ya kusomesha msomaji moja kwa moja misingi ya maisha ya kijamii kwa kuonyesha jinsi wahusika wazuri walivyotuzwa na jamii na maisha ya wahusika wabaya kuadhibiwa.

Jukumu hili linaafikiana na lile la Fasihi Simulizi iliyosisitiza maadili mema katika jamii.Maudhui ambayo Shaaban Robert ameyapa kipaumbele katika Riwaya ya *Utubora Mkulima*. Riwaya hii imesheheni athari za kimtindo za fasihi simulizi tangu mwanzo hadi mwisho. Riwaya hii inaanza kwa mtindo wa kisimulizi kwa mfano (1968:1) "Baada ya kutoka Burma, siku moja..."

Athari zingine za kimtindo ni ugawaji wa riwaya ya *Utubora Mkulima* katika mada ndogo ndogo kam vile, *Kuacha kazi, Nuru Ndogo, Bihaya* na kadhalika na kisha mwandishi kutoa maelezo yanayohusu kila mada. Mtindo huu unadhihirisha athari za fasihi simulizi. Hali kadhalika athari hizi za fasihi simulizi zinaonekana mwishoni mwa riwaya hii ambapo Shaaban anakamilisha kwa kuandika, (1968:91) "Hapa ndipo pahali pa kuishia hadithi hii..." mbinu ambayo hutumika sana katika kutamatisha hadithi katika Fasihi Simulizi.

Matumizi ya tamathali za lugha kama vile methali, tashbihi, taswira, mbinu rejeshi, kinaya taharuki na kadhalika ni sababu tosha kuwa riwaya ya *Utubora Mkulima* imeathiriwa kwa kiwango kikubwa na fasihi simulizi.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA

Uhakiki wetu umejifunga katika athari za fasihi simulizi katika riwaya ya *Utubora Mkulima.*

Tutaweka bayana mifano mwafaka ya athari za fasihi simulizi katika riwaya ya *Utubora Mkulima* katika utafiti wetu ili kudhibitisha lengo letu la utafiti.

## 1.6 MISINGI YA NADHARIA

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya vikale.

Kwa mujibu wa Wafula R.M na N. K. (2007:106), Vikale ni picha kongwe zinazotokea mara kwa mara katika kazi za fasihi. Vikale hivi vinaweza kuwa taswira, wahusika, miundo ya usimuliaji na fani zingine zinazopatikana katika fasihi yoyote.

Abrahams (1971:11-12), alieleza nadharia ya uhakiki wa vikale kwa mitazamo miwili. Alieleza kuwa chimbuko la nadharia hii ni kutokana na kazi ya James G.Frazer katika kitabu cha "*The Golden Bough*" (1890-1915) kilichotolewa na katika idara ya Antropolojia Linganishi, Chuo Kikuu cha Cambridge. Abrahams (1971:11-12) aneleza kuwa kitabu hiki kilifuatilia ruwaza za kimsingi za visaasili na za kitambiko ambazo alidai hujirudiarudia katika visakale na taratibu nyingi katika tamaduni anuwai. Kwa upande mwingine alieleza kuwa, nadharia ya vikale ilitokana na maelezo ya Carl G. Jung kuhusaina na akili-laza. Jung alikuwa mwanafunzi wa Sigmund Freud, mtaalamu aliyeasisi taaluma ya uchanganuzi nafsia. Lakini walitofautiana kimawazo. Wakati ambapo Freud alisisitiza akili-laza ya kibinafsi, naye Jung alisisitiza kuhusu akili-laza jumuishi. Jung alitumia istilahi ya vikale kwenye taswira za asili za kumbukumbu zinazorudiwarudiwa kutokana na tajiriba katika maisha ya tangu mababu zetu wa kale. Alisisitiza kuwa, taswira hizi hurithiwa na kutiwa kwenye akili-laza jumuishi ya jamii ya watu na ambazo hudhihirika katika visaasili, ndoto, mawazo ya binadamu mathalan, katika vipengele vyote katika maisha ya binadamu wote duniani na pia katika kazi za kifasihi. Katika uhakiki wa kifasihi, vikale hutumiwa katika ruwaza ya aina za wahusika au taswira ambazo zinafanana katika tungo mbalimbal za kifasihi na pia katika visasili na mitindo anuwai ya kijamii. Kufanana katika maswala haya anuwai huchukuliwa kuakisi seti ya ruwaza bia ambazo zimekuwepo tangu

jadi. Nadharia ya uhakiki wa vikale kwa hivyo inaeleza kuwa binadamu wote ni sawa popote walipo. Tofauti ni kidogo za kufikirika ambazo husababishwa na tofauti za kihistoria na za kimazingira.

Kwa mujibu wa Mutiso (1999:2). Kwa jumla, vikale hurejelea ruwaza za kimsingi. Ruwaza za jumla au bia za aina moja au nyingine ambazo aghalabu hudhihirika katika jamii za watu mbalimbali duniani. Anashikilia kuwa vikale humvuta msomaji vikitumiwa vizuri katika kazi ya fasihi.

Waitifaki wa nadharia ya vikale wanashikilia kwamba umaarufu wa kazi ya sanaa unatokana na wahusika, maudhui na taswira zinazorudiwarudiwa katika kazi husika. Baadhi ya wahusika wanaotumiwa kudhihirisha vikale ni kama: jaribosi au nguli anayeandaa safari ambayo mara nyingi huanzia utotoni hadi anapofika utu uzima ambapo safari hii inaweza kuwa ya kikweli pale nguli anajizatiti kukisaka kitu au kujisaka mwenyewe. Katika nadharia ya vikale, mkinzani wa nguli huwa ni mhusika wa kikale ambaye hujifunga kibwebwe kuiharibu mipango ya nguli kwa kujaribu kumwangamiza. Aghalabu mhusika huyu huwa mzinzi, mlafi na wakati mwingine huwa tajiri. Hii inaafikiana na sifa za Mkinzani wa mhusika mkuu Utubora katika riwaya hii ambaye ni Makuu.

Mpenzi ni kikale, anaweza kutokea kwa sababu ya kumrubuni nguli asiweze kutekeleza mradi wake. Kwa mfano Sheha aliyekuwa mpenzi wa Utubora anafanya kila juhudi ili Utubora asiipate kazi kwa babake, Ahmed wala asiweze kumuoa Radhia na badala yake amuoe yeye.

Vilevile katika nadharia hii ya vikale mzee mwenye hekima hutokea ili kumwasa nguli ambapo hutumia miujiza au uramli kumsaidia nguli. Katika riwaya ya *Utubora Mkulima*, Bi.Mkubwa anapofariki anamrithisha Utubora mali yake yote kupitia kwa wasia wake.

Pamoja na kutumia wahusika, mkabala wa nadharia ya vikale huangazia maudhui ya wema na uovu miongoni mwa mengine katika jamii kama alivyofanya Shaaban Robert katika riwaya ya *Utubora Mkulima.*

Katika utafiti huu tutatumia mtazamo wa mtaalamu Gustav Jung kwa kumuonyesha Shaaban Robert anavyomsawiri Utubora katika safari ya kuijenga jamii adilifu kuonyesha maudhui ya wema na uovu na jinsi mhusika huyu anavyopambana na vipingamizi kutoka kwa wakinzani wake, Makuu na Sheha.

Haya yote ni katika kudhihirisha kuwa fasihi andishi ni picha kongwe za fasihi simulizi au athari za fasihi simulizi zinazotokea mara kwa mara katika fasihi andishi.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO LA UTAFITI

Zaja J.O (1986), katika tasnifu yake ya uzamili alishughulikia fasihi tafsiri katika ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili: matatizo na athari zake alieleza kuwa, hadithi na hekaya za Kiarabu pia zilitafsiriwa na kuingizwa katika fasihi ya Kiswahili kama vile mazungumzo ya *Alfu Lela- Ulela* na *Hekaya za Abunuasi*. Kulingana na Zaja, kupitia kwa tafsiri hizi athari za kimaudhui na kiumbo ziliingia katika fasihi ya Kiswahili na baadaye zikawaathiri watunzi wa Kiswahili kama vile M.S.Farsy katika *Kurwa na Doto* na Shaaban Robert katika *Adili na Nduguze*.

Maoni haya ya Zaja yamechangia katika utafiti wetu kuhusu athari za fasihi simulizi katika riwaya ya *Utubora Mkulima,* kwani swala la maadili limechukua nafasi kubwa katika riwaya ya *Utubora Mkulima* na hii ni athari itokanayo na fasihi simulizi. Zaja anaendelea kueleza katika tasnifu yake kuwa, kabla ya Fasihi Simulizi kuingiliwa na athari za kigeni kutoka ng'ambo, ilikuwa ni fasihi ya kusimuliwa tu, kama zilivyokuwa fasihi zote za Kiafrika.Fasihi simulizi katika tanzu zake kama ngano, hekaya, hadithi vitendawili na nyimbo ilisawiri harakati za watu katika fani mbalimbali za maisha.

Kando na Zaja J.O, Mbatia M. (1999), katika tasnifu yake ya shahada ya uzamifu alituelezea historia fupi jinsi dhamira ya maadili ilivyokuja kutokea katika kazi za kinathari za Shaaban Robert. Mbatia alieleza kuwa, dhamira ya maadili ilitawala sehemu kubwa ya fasihi simulizi kwa sababu mojawapo ya malengo ya fasihi simulizi ni kuhimiza maadili miongoni mwa watu katika jamii.

Mbatia alifafanua kuwa, kwa vile Shaaban anaweza kuchukuliwa kuwa mwasisi wa fasihi ya kubuni ya kinathari ya Kiswahili, ni mwandishi wa kwanza wa riwaya ya Kiswahili ambaye ameathiriwa na elementi ya kimaadili ya Fasihi Simulizi. Mbatia anaendelea kusema kuwa, kazi za mwanzo za kibuni za Shaaban Robert zina uwiano mkubwa na Fasihi Simulizi.

Maoni haya ya Mbatia, yanachangia kikamilifu katika utafiti huu kuwa kuna athari za fasihi simulizi katika riwaya ya *Utubora Mkulima* hasa anapoarifu Mbatia kuwa, vilevile Shaaban alikuwa ameathiriwa na fasihi simulizi iliyotafsiriwa hadi Kiswahili hususan mazungumzo ya *Alfu Lela-Ulela.* Alisema kuwa hadithi hizi zilidhihirisha adhabu kali kwa watovu wa maadili.

Vilevile Seif Kiango anakiri kuwa fasihi simulizi ni chemchemi ya fasihi andishi ila hajaweka wazi viunzi ambavyo ni vya fasihi simulizi katika fasihi andishi. Utafiti wetu umeweka wazi vipengele hivi katika riwaya ya *Utubora Mkulima* kimoja baada ya kingine.

Mbughuni (1978), katika tasnifu yake ya shahada ya uzamifu: From Oral to Written. The Politicization of Kiswahili Literature in Tanzania alituarifu kuwa nathari za kubuni za Kiswahili nchini Tanzania zilianza wakati wa serikali za kikoloni ambapo kulikuwa na haja ya kutosheleza malengo ya kielimu. Maandishi ya kwanza ya kinathari yalikuwa na sifa za Fasihi Simulizi na kwa vile kazi hizo zilikuwa na malengo ya kielimu ziliyamulika zaidi maswala ya maadili.

Maoni haya yanaunga mkono mtazamo wa utafiti huu kuwa riwaya ya Utubora Mkulima ina athari za fasihi simulizi kwani ni mojawapo ya kazi za kinathari za mwanzo za Shaaban Robert na suala la maadili analolipa kipaumbele lina mizizi yake katika fasihi simulizi

R.M. Wafula (1989), katika tasnifu yake ya uzamifu, ameshughulikia majazi katika riwaya za *Utubora Mkulima, Adili na Nduguze* na *Siku Ya Watenzi Wote*. Alisema kuwa Shaaban alidhihirisha mtazamo wa kidini kuwa kazi ni staha na agizo kutoka kwa Muumba na ni jukumu la binadamu kuitenda. Dini ni mojawapo ya nguzo za Fasihi Simulizi na athari hizi zimebainika katika riwaya ya *Utubora Mkulima* na kuchangia kwa kiasi kikubwa tatizo letu la utafiti ambalo linahusu *athari* za fasihi simulizi katika riwaya ya *Utubora Mkulima.*

Mbatia.M. (1990), alichanganua mbinu za uandishi katika riwaya za mwanzo za Shaaban Robert, kazi hii imechangia katika utafiti wetu katika kuhakiki mikakati ya uandishi iliyotumika katika riwaya ya*Utubora Mkulima*.

Mwandawiro J.D.M (1984), ameshughulikia suala la fasihi simulizi katika jamii. Alisema, "Mbele binadamu walianza kuwasiliana kwa vitendo na kwa mazungumzo. Fasihi mazungumzo, yaani fasihi simulizi, ndiyo shina na mizizi ya fasihi andishi". Tumelitoa wazo hili muhimu kuthibithishia kuwa fasihi andishi ni zao la fasihi simulizi, hivyo basi kwa vyovyote vile ina athari kubwa katika fasihi andishi na hasa riwaya ya *Utubora Mkulima*

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Kimsingi utafiti huu umekuwa wa maktabani. Tumezisoma tasnifu kadha wa kadha zilizoshughulikia athari za Fasihi Mimulizi katika riwaya za Kiswahili , vilevile tumezitumia hoja za hapa na pale zilizotolewa na waandishi wa vitabu vya fasihi simulizi pamoja na riwaya za Kiswahili kwa madhumuni ya kubaini namna vipengele vya fasihi simulizi vinavyothiri kazi za kubuni za riwaya.

## 1.9 KIMALIZIO

Katika sura hii, tumeshughulikia tatizo la utafiti kwa kubainisha athari za fasihi simulizi katika riwaya ya *Utubora Mkulima*. Aidha tumepitia kwa muhtasari baadhi ya tafiti za awali ili kubainisha pengo la utafiti.

Tumepiga hatua zaidi na kubainisha madhumuni na nadharia tete ambazo zimekuwa jira ya utafiti wetu. Tumetoa ithibati kuhusu sababu zilizochangia uchaguzi wetu wa tatizo linalotafitiwa pamoja na upeo na mipaka ya utafiti wetu.

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya vikale. Tumejadili mihimili ya nadharia hii na kuonyesha ufaafu wake katika utafiti wetu.

Tumetalii yalioandikwa kuhusu tatizo la utafiti na kutamatisha kwa kuangazia nyenzo za utafiti ambazo ni mwafaka katika utafiti wetu.

## SURA YA PILI

## MAISHA YA SHAABAN ROBERT

### 2.0 UTANGULIZI

Shaaban Robert ni mwandishi mtajika katika fasihi ya Kiswahili. Maandishi yake mengi ni katika utanzu wa ushairi, hata hivyo, vilevile ni mwandishi hodari wa riwaya za Kiswahili.

Shaaban Robert aliandika wakati na baada ya ukoloni nchini Tanzania. Mwandishi huyu amechukuliwa kama kiunzi kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi, kwani aliandika mashairi kadha na ambayo huanishwa katika vipera vya fasihi simulizi kama vile utenzi wa *Hati* na Utenzi wa *Adili.*

Kwa mujibu wa utangulizi katika tawasifu yake *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* "Shaaban Robert ndiye aliyekuwa mmojawapo wa waandishi wa kwanza kuandika kuhusu utamaduni na elimu ya kimaadili na mwanazuoni wa elimu na lugha ya Kiswahili."

Gibbe A.G. (1980:2), Anasema "Maandishi yake yako katika sehemu mbili: nathari na ushairi."

### 2.1 MAISHA YA SHAABAN ROBERT KWA UFUPI

Shaaban Robert alizaliwa tarehe moja Januari 1909 Vibambani, kijiji kilicho kusini ya Machui yapata maili sita kutoka Tanga nchini Tanzania.

Baba yake aliitwa Robert Juma Ufukwe, naye mama yake aliitwa Mwema Binti Mwidau. Wazazi wake walimpenda na kumwamini Shaaban Robert hata wakamsimulia mambo mengi

yahusuyo mila na desturi za jamii yake. Jina la asili Ufukwe, lilitokana na ufuo wa bahari mahali alipozaliwa. Wazazi wake walikuwa wa ukoo wa Mganga wa kabila la Kiyao.

Robert ni jina la Mjerumani aliyekuwa mwajiri wa baba yake Shaaban. Wazazi wa Shaaban walitalakiana muda mfupi baada ya Shaaban kuzaliwa.

Shaaban alisomea shule ya Msimbazi, Dar es Salaam kuanzia mwaka 1922 hadi 1926. Kisomo cha Shaaban cha darasani kilikuwa kidogo sana. Katika wanafunzi kumi na mmoja waliofuzu mtihani chuoni, alikuwa mtu wa pili na kupewa cheti cha kutoka chuoni yaani "School Leaving Certificate."

Kwa mujibu wa Gibbe A.G. (1980) akimnukuu J.W.T.Allen "Kutokana na juhudi zake, alielimika zaidi na kuivuka mipaka ya kisomo alichopatiwa na wakoloni."

Baadhi ya waandishi wanaeleza kuwa Shaaban alioa mara tatu. Kwa mujibu wa Gibbe A.G.- *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1949: vi), Shaaban Robert alioa mara tatu, ilhali waandishi wengine wanadai alioa mara mbili.

Mkewe wa kwanza aliyemchumbia kwa miaka kumi na hatimaye kumuoa, aliitwa Amina. Amina alifariki baada ya kuugua na kumwacha Shaaban na watoto wawili, msichana na

mvulana. Baada ya miaka mitano ya ujane, Shaaban alimwoa mke wake wa pili aliyemchumbia kwa miaka miwili.

Serikali ya mkoloni katika kumwajiri Shaaban Robert ilikuwa na nia ya kumtumia tu kama chombo cha kunyonyea Waafrika. Kwa mujibu wa Gibbe A.G. (1980: 1),"Wakoloni walimrubuni kwa kumpandisha cheo, ili wamfanye chombo cha kunyonyea. Alipandishwa cheo kuwa Grade III Higher Division, 1929, baadaye akawa Grade II Local Civil Service. Kutokana na juhudi zake aliweza kuwa mwanachama wa:

a) East African Swahili Committee

b) East African Literature Bureau

c) Tanganyika Language Board

d) Tanga Township Authority (Baadaye Town Council)

Shaaban Robert baada ya kutoka shuleni, aliajiriwa kama karani na serikali ya mkoloni na kufanya kazi katika idara mbalimbali. Huku akionyesha ufanisi mkubwa katika kila kazi aliyoifanya.

Kwa mujibu wa diwani yake *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini,* (1949: iv), Shaaban Robert alifanya kazi Forodhani Pangani na mahali pengine kutoka mwaka 1926 hadi 1944.

a. Idara ya wanyama kutoka mwaka 1944 hadi 1946;

b. Afisi ya mkuu wa jimboTanga kutoka mwaka 1946 hdia 1952.

c. Afisi ya usoroveya Tanga 1952 hadi 1960.

Pia Shaaban Robert alikuwa mwanachama wa mashirika mbalimbali. Kufanya kazi katika idara mbalimbali hakukumpa umaarufu Shaaban Robert Kama kazi yake ya uandishi.

Kwa mujibu wa Gibbe A.G. (1980:2), "Kazi iliyompa jina si ya uanachama au ukarani ila ni kazi ya uandishi."

Senkoro (2011:98), alisema ya kuwa Shaaban Robert alifariki tarehe 20 Juni 1962, akatuachia hazina kubwa sana katika uwanja wa Fasihi ya Kiwahili ya jumla ya vitabu vyake 24 ambavyo vinafahamika na vimechapishwa.

## 2.2 KAZI ZA KINATHARI ZA SHAABAN ROBERT

Kwa mujibu wa Gibbe A.G. (1980:2), kazi za kinathari za Shaaban Robert ni zifuatazo:

1. *Maisha Yangu na Bada ya Miaka Hamsini*, 1936 na 1946

   Nelson 1949

2. *Kusadikika*, 1948, Nelson 1951
3. *Adili na Nduguze* 1951, Macmillan 1952, TPH, 1977
4. *Kielekezo cha Insha*, 1951-1953, Witwatersrand 1954.

   Oxford 1966

5. *Wasifu wa Binti Saad*, 1958, Arts & Literature, Nelson 1967
6. *Kufikirika*, 1946-1947, Oxford 1968

7. *Utubora Mkulima*, 1960-1961, Nelson 1968

8. *Siku Ya Watenzi Wote*, 1960-1961, Nelson 1968

Haya ndiyo maandishi ya Shaaban Robert tunayoyafahamu ila yawezekana kuna mengine ambayo bado hayajagunduliwa yalipo wala kuchapishwa. Maandishi haya yanatufunulia fikra zake Shaaban Robert kuhusu malimwengu na walimwengu wenyewe wa wakati wake, na ni hazina ya mafunzo kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Kwa Mujibu wa diwani yake (1949:v), *Maisha Yangu na Baada Ya Miaka Hamsini*, alikuwa mshairi maarufu zamani zake katika gazeti la *Mambo Leo*, kila aliyelisoma hakukosa kupata fundisho fulani kwa tungo hizo. (1949:67), "Bahati ilinifanya mshairi tangu 1932."

Shaaban aliacha kazi ilipolazimu mwaka wa 1959. Rafiki yake mzungu alimtunukia kalamu ya maagano, labda ulikuwa ni wito kwa Shaaban Robert ambaye alikuwa amestaafu kufanya kazi kwa serikali ya mkoloni aendelee na uandishi, kipawa ambacho mkoloni alikuwa ameshakitambua.Shaaban Robert aliendelea na uandishi wake.

Katika mwaka wa 1936, wakoloni waliandaa mashindano ya uandishi wa insha yalioitwa *East Africa Literary Composition Competition* ambapo Shaaban Robert aliwasilisha mswada uliohusu maisha yake na baada ya miaka hamsini, ambapo aliibuka mshindi. Shaaban alituzwa kwa zawadi ya waandishi inayoitwa 'Margaret Wrong Prize" na pia kupewa nishani ya M.B.E. Uandishi wake ni kivukio cha fasihi za kale na fasihi za sasa.

Shaaban Robert aliaga dunia tarehe 22 Julai 1962 akiwa ameacha hazina kubwa ya mashairi, riwaya na insha zenye maudhui ya kimaadili. Alizikwa Machui.

Kwa mujibu wa Senkoro (1999:99), "Shaaban Robert ni mmoja wa waandishi ambao daima wameshughulikia binadamu na matatizo yake."

## 2.3 FALSAFA YA SHAABAN ROBERT

Kamusi ya karne ya 21: inaeleza Falsafa kama taaluma ya nadharia za maana ya vitu, kwa mfano, maisha, maarifa, imani asili yake na sababu za kuwepo kwao.

Falsafa ni busara inayofikiwa na mtu baada ya harakati za kutafakari juu ya jambo au mambo yoyote ya kilimwengu. Binadamu aghalabu hufikia msimamo wake katika maisha baada ya kutafakari sana na kupata busara na mantiki fulani katika maisha.

Kwa mujibu wa Njogu K. na Chimerah R. (1999:48), Falsafa ni busara iliyofikiwa baada ya mtu au watu, kutafakari kwa kina kuhusu jambo lolote la kilimwengu. Ni busara itokanayo na harakati za kimawazo

Ni muhimu kufahamu kuwa, ingawa mwandishi huenda akawa na falsafa pana iliyopenya vipengele mbalimbali vya maisha, atakuwa na falsafa zingine ndogondogo zitakazojitokeza

katika maandishi yake.Hizi falsafa ndogondogo ndizo zitakazoijenga na kuimarisha falsafa yake pana.

Lakini falsafa hii ya mwandishi hutokana na utazamaji wake wa yale yanayojiri katika jamii yake kisha akayatafakari akiwa peke yake au na wenzake. Mtazamo wake utaathiriwa na mazingira yaliyomlea na kumkuza, Kwa mfano mwandishi aliyekulia katika mazingira ya kidini atabainisha athari za dini katika maandishi yake.

Shaaban Robert alianza kuandika riwaya zake wakati Tanganyika ikiwa chini ya himaya ya mkoloni. Aidha dini za kikristo na kiislamu zilikuwa zimepenya sehemu nyingi za bara Afrika na zikayaathiri maisha ya wenyeji na misimamo yao.Isitoshe, mfumo wa kikoloni ulitisha na kuogofya hivi kwamba mwandishi aliyepungukiwa na ujasiri hangetangaza msimamo wake waziwazi kwa kuhofu kudenguliwa na walowezi.

Msimamo wa Shaaban Robert haukuwa wa kiharakati kikamilifu kwa sababu kama asemavyo katika shairi lake liitwalo woga katika diwani yake *Kielezo cha Fasihi*. Shaabani Robert anahisika kuunga mkono utawala wa mkoloni hasa anavyomsifu kiongozi mkoloni anapowatembelea wenyeji.

Athari hizi za kijamii na waandishi wengine zilimwaathiri Shaaban Robert katika falsafa yake ya udhanifu, na hatimaye kumtosa katika bahari ya dunia ya kidhahania au utopia .Maandishi yake mengi yenye maudhui ya kisiasa na kijitimai, yamelenga kwenye falsafa ya udhanifu. Maandishi ya Shaaban Robert yamelenga hulka za binadamu zinazomtafautisha na mnyama.

Katika riwaya ya *Utubora Mkulima,* Shaaban Robert amemsawiri mhusika Utubora Mkulima kwa ufasaha kabisa ili falsafa yake kuhusu utu bora ipate kueleweka kwa hadhira yake. Kazi hii ni kioo cha jamii katika kujiangalia na kujiona iishivyo, inavyotaka kuishi na anavyopendekeza Shaaban jamii iishi kulingana na dhamira ya riwaya *Utubora Mkulima.*

Kwa kuzisoma kazi zake hasa *Utubora Mkulima,* tunabainikiwa vyema na suala la utu bora na falsafa nyingine zinazohusu maisha ya binadamu. Mhusika Utubora amechorwa kama kielelezo cha kile Shaaban Robert akionacho kama utu bora.

Masimulizi ya mwandishi aghalabu yatatokana na upekuzi na uteuzi wa hali mbalimbali zinazogusa hisia zake, upekuzi na uteuzi wa hali zitakazosimuliwa mara nyingi huwa zinafungamana na falsafa yake kuhusu yale ayaonayo.

Kwa mujibu wa Njogu K. na Chimera R. (1999:49), “Falsafa ya binadamu yeyote ni sharti iwe na misingi yake katika jamii ambayo mengine yanayohusiana na wanajamii wawa hawa.

Mbali na athari zinazotokana na waandishi wengine mazingira, matukio ya kihistoria, mtazamo wa kibinafsi, dini, imani, utamaduni na kadhalika huchangia pakubwa falsafa ya msanii.

Msimamo wa Shaaban Robert ulidhihirika pale mtazamo wake kuhusu wanawake ulipingana na ule wa dini na utamaduni kuhusu utawishaji wa wanawake, Shaaban aliushikilia kabisa msimamo wake wa usawa wa kijinsia. Shaaban alionelea kuwa utamaduni wa Kiafrika ulimuonea sana mwanamke na akalipinga hili kwa dhati na kuelekeza jinsi mwanamke

anavyopasa kuchukuliwa katika jamii. Alikashifu utawishaji wa wanawake uliofanywa na dini na utamaduni kwa kudai kuwa utawa ulimnyima mwanamke nafasi ya kujitegemea na kunyanyaswa na mwanaume.

Shaaban anamsawiri Binti Saad kama kielelezo cha wanawake bora katika maandishi yake ya nathari ya *Wasifu wa Binti Saad* (1958), anamsawiri Binti Saad kama mwanamke aliyejinasua kutokana na kunyanyaswa na kumtegemea mwanamme, na kwa juhudi zake, alikitumia kipawa chake cha uimbaji na uigizaji kujikimu kimaisha. Hii ilikuwa ni kinyume na matakwa ya dini na utamaduni wa jamii yake ambao ulimdhalilisha mwanamke. Dhana hii ya udhalilishaji wa jinsia ya kike ina misingi yake katika fasihi simulizi, ndani ya utamaduni ambao ni jumla ya maisha katika jamii yoyote ile. Fasihi Simulizi kamwe haiwezi kutenganishwa na jamii, na athari zake kama vile udhalilishaji wa kijinsia ni baadhi ya maswala yanayoshughulikiwa na fasihi andishi. Athari hizi za fasihi simulizi hasa ndicho kiini cha udhalilishaji wa jinsia ya kike ambao umechochea uandishi wa riwaya nyingi za Kiswahili.

Kimsingi, Shaaban Robert alisisitiza sifa za utu bora. Suala la utu linajitokea wazi katika riwaya yake ya *Utubora Mkulima* kupitia kwa nguli wake Utubora. Utu bora umefungamanishwa na bidii ya kutenda mambo ya ujasiri, haki ukweli na heshima. Shaaban anamsawiri Utubora kama mhusika aliye na sifa nyingi zinazoenziwa na jamii.

Shaaban Robert (1968:1) anamweleza Utubora Mkulima ifuatavyo

> Utubora alikuwa mtu imara mbele ya telezi nyingi kama vile
> hiana na mengineo. Mvumilivu mbele ya majaribu magumu,

> kama rushwa! Hodari mbele ya mashaka mazito, mfano wa
>
> kushika amana au dhima kubwa: mwaminifu kama mchana:
>
> na msiri kama usiku. Kwa kushika majira alikuwa kama saa:
>
> na mahudhurio yake mema katika kazi hayakuwezekana
>
> kushindwa na watumishi wengine.

Kila siku yeye alikuwa mtu wa kwanza kuhudhuria kazini wakati wenziwe walipokuwa wamechelewa na wa mwisho kuondoka kazini, wakati wengine walipotangulia kwenda zao."

Shaaban anatukuza sifa za Utubora kama vile bidii, uvumilivu, uaminifu na utu akiamini kuwa ndiyo maadili yatakayoleta maendeleo na heri njema katika jamii.

Athari hizi zimetokana na fasihi simulizi, ambapo jamii katika hadithi zake ilinuia kufunza wanajamii umuhimu wa maadili haya kwa kutumia wahusika wanyama au binadamu.

## 2.4 KUHUSU FEDHA

Shaaban Robert anauweka msimamo wake wazi kuhusu fedha, kuwa si kila kitu katika maisha. Utu ndicho kitu muhimu kwa binadamu. Hili linabainika anapomwachisha Utubora kazi ya mshahara mkubwa. Shaaban Robert (1968:1)

> mshahara wake Utubora ulikuwa simulizi karibu
>
> katika Unguja nzima, ilisemwa pia kuwa uliwatia wivu

watu wengi sana. Alianza kazi kwa mshahara wa shilingi 100 kwa mwezi. Baada ya miaka mitano tu, alifika mshahara wa shilingi 500 kwa mwezi kabla ya kwenda Burma. Aliporudi Unguja alishika tena kazi yake ile ile kwa mshahara wa shilingi 1,000 kila mwezi. Hata katika afisi za serikali hapakuwa na karani alikuwa anapata mshahara mkubwa kama huo.

Ukurasa 52 "...Sidhani kuwa fedha huweza kukidhi matilaba yote ingawa mtu lazima kuwa na kiasi fulani cha fedha ya kumsaidia na kumpatia mahitaji ya kawaida..." "Basi kutia utumwani maisha ya mtu kwa sababu ya kupata fedha ni jambo nisiloweza kuvumilia"

Pamoja na sababu zingine kama vile kuachwa na mpenziye Sheha na kifo cha mamake mpendwa, zilizomfanya Utubora kuacha kazi, Shaaban Robert amemsawiri mhusika wake kwa namna ya kutubainishia kuwa pesa si kila kitu katika maisha. Alitukuza maadili dhidi ya pesa au utajiri pale anapomwoza Radhia kwa Utubora na kumwacha Makuu ambaye alikuwa na pesa.

Shaaban Robert aneleza kwamba, fedha haipaswi kumwondolea mtu ubinadamu na haki zake, Shaaban Robert ameonyesha kwamba ndoa isifungamanishwe na mali, bali ifuate hisia za maharusi. Sheha anamtaliki mumewe tajiri, ingawa anatumia fedha ili ziwe chambo cha kumnasia Utubora lakini hafanikiwi. Shaaban Robert anatuonyesha ulimwengu ambao itikadi zake na nyendo zake zimetawaliwa na fedha. Watu wameutweza utu na kutwaza mali. Utajiri

unaonekana ndio msingi wa maisha, hata kama utajiri huo umepatikana kwa udhalimu. Mfano, Makuu anaamini kwamba bila fedha mwanaume hawezi kuoa hata mwanamke anayempenda. Vilevile mamake Radhia anamshauri bintiye amchague mwanamme aliye na mali kabla ya kukubali posa na hatimaye kuolewa.

Katika kisa hiki, Shaaban anaweka wazi ukweli kwamba utu unapiku mali na ndipo Radhia ambaye alitoka katika familia tajiri aliamua kuolewa na mkulima wakawaida. ukulima huu ulioonekana kuwa duni katika jamii. Hii ilikuwa kinyume na matakwa ya wazazi wake waliomtaka binti yao Radhia aolewe kwa tajiri mwenza Makuu.

Huu ni mwendelezo wa yale yaliyosisitizwa na Fasihi Simulizi kuwa maadili ni 'dhahabu' kwa binadamu aliyenayo. Athari hizi zimemwandama mwandishi Shaaban Robert katika uandishi wake wa riwaya *Utubora Mkulima*. Hili ndilo lengo kuu la utafiti wetu, kuonyesha athari za Fasihi Simulizi katika uandishi wa riwaya ya Shaaban Robert (1968).

## 2.5 KUHUSU DINI

Ili kutudhihirishia kuwa Shaaban Robert katika riwaya ya *Utubora Mkulima* amekita mizizi katika dini, anatusawiria jumuia ya adili ambayo ndiyo kilele cha falsafa yake. Hapa ndipo mwandishi huyu anajitokeza kama mwandishi aliyepaa hadi kwenye falsafa ya udhahania yenye misingi katika itikadi za dini. Falsafa ya kidini hasa dini ya Kiislamu ilimwathiri sana Shaaban Robert. Alizingatia mambo mengi katika uandishi wake yaliyosisitizwa na dini hasa ya Kiislamu na utamaduni wake.

wenyewe. Hali hii ya kidini imemwadhiri Shaaban katika mtazamo wake hasa anapoandika kutumia mtazamo wa kidhanifu kuhusu ujenzi wa jamii mpya (1968: 64), anasema "Naamini kuwa mwisho uungojao utakuwa ndio mwanzo hasa wa maisha yaliyo kamili na bora."

Kwa ajili ya athari za dini ya Kiislamu ambayo kwayo Shaaban Robert ni muumini, yeye haamini kuwa kuna kifo, kumhusu marehemu mamake Shaaban Robert anasema, (1968:62), "....la hakufa wala hapana kitu kifacho kamwe." Hali hii inatokana na imani ya dini kuwa mtu aliyeamini katika Muumba anapokufa huwa amelala akisubiri siku ya kiama. Katika falsafa hii ya kidini, Shaaban anaona ni kazi bure kutafuta furaha katika maisha haya. Furaha kamili hupatikana akhera bdiposa alipopata mashaka alieleza (1968:63), "Kutafuta furaha katika maisha ni kama kutafuta paka mweusi katika chumba chenye giza."

Dondoo hizi zinadhihirisha kuwa Shaaban Robert aliathirika na mafunzo kuhusu dini hasa ya Kiislamu na kuyafanya maandishi yake yawe ya Kiutopia. Jamii mpya anayoikusudia ni jamii ya siku ya kiama ambapo kila mtu mwema atatuzwa ilhali mwovu ataadhibiwa. Hili linamfanya mwandishi Shaaban Robert kuonekana kama asiye mwanaharakati wa kimapinduzi katika jamii iliyokuwa inakandamizwa chini ya utawala wa mkoloni, akihimiza: upendo, utiifu au heshima na utubora kwa mkoloni kutoka kwa mwafrika

## 2.6 KUHUSU NDOA

Falsafa ya Shaaban Robert kuhusu ndoa ni kuwa arusi yenye misingi ya fedha haidumu bali huvurugika. Anatupatia mfano wa Sheha na mumewe tajiri. Anamshauri kuwa utu bora una

mizizi katika kuwathamini watu kwa sababu ni watu bila kuzingatia matabaka yao. Ndoa yenye usawa kati ya mume na mke hudumu.Shaaban Robert anamsawiri Binti Saad akikataa kuthamini mila na dini na kumwacha mumewe na watoto na kujitosa mjini na kujitafutia riziki pasipo kudhalilisha utu wake.

Binti Saad alivikuza vipawa vyake na kujikomboa kutoka kwa pingu za utamaduni. Kinyume na utu anaoushikilia Shaaban, hiari ya Binti Saad kutoikimu jamii yake ilhali pato analo inautia kasoro utu wake Binti Saad.

## 2.7 ATHARI ZA WAANDISHI WENGINE

Hakuna msanii anayeibuka na kuandika kutoka ombwe tupu, aghalabu huwa anachota kutoka kwa wasanii wenzake waliomtangulia au wa wakati wake.

Chambilecho Gibbe A.G. (1980:3), "Tukitaka kumuelewa vizuri Shaaban Robert hatuna budi tuwaelewe kwanza kwa makini mabingwa waliomtangulia. Tukichunguza kwa makini ushairi wa Kiswahili kutoka kale, tutaona kuwa maandishi na mawazo ya Shaaban Robert ni mwendelezo na pengine marudio ya maandishi na mawazo ya mabingwa hao. Kwa mfano, *Al- Inkishaf* (1720-1820) yake Seyyid Abdalla Bin Nassir, aliouandika kuonya kuwa kuna mioto mikali kwa wale watakaoasi mafunzo ya utenzi huo baada ya kufa. Utenzi huu unamwathiri Shaaban Robert kwa kina hususan anapoandika, (1980:3), "Shaaban Robert alipotunga '*Marudi Mema*' maudhui yalikuwa sawia na ya *Al-Inkishafi.*"

Shaaban Robert baada ya kufiwa na mkewe wa kwanza na kuachiwa watoto, aliwaandikia tenzi *'Hati'* na *'Adili'* kwa bintiye na mwanawe mtawalia kwa madhumuni ya kuwaongoza. Vile vile maudhui katika tenzi hizi mbili ni sawa na utenzi wa *Mwana Kupona* (1841-1933) naye Mwana Kupona Binti Msham kwa ajili ya binti mwana Heshima binti Sheikh, baada ya kuugua mwaka mzima na kuhofu kuwa huenda angefariki na kumwacha bintiye bila malezi.

Madumulla J.S (2009:42) anasema ya kuwa, "Nathari tangulizi inayojulikana kuandikwa na mwenyeji ni *Habari za Mrima* iliyoandikwa na Sheikh Ali Bin Hamed, mnamo mwaka 1880. Shaaban Robert alikuwa mmoja wa waandishi wa awali mwenyeji wa riwaya za kinathari aliyeathiriwa na riwaya za awali za kisafari na maadili na kitawasifu.

Hizi ni ithibati ziinazoipa mashiko kazi yetu ya utafiti kuwa kuna athari si haba za fasihi simulizi katika maandishi ya Shaaban Robert hususan *Utubora Mkulima*.

Kulingana na Ogechi O. na wenzake (2008:94), "….Hawa waandishi katika maandiko walitumia ujumi uliofanana sana na hiyo Elimu Kuu ya Kiulaya ya karne ya kumi na nane. Maandiko yao yalikuwa ni ya kielekezi yalilenga zaidi madhumuni ya kumsomesha msomaji moja kwa moja misingi ya maisha ya kijamii. Waandishi hawa ni Shaaban Robert, J. Kiimbila, Naila Harusi, Leo Omollo na wengine. Lengo lao lililingana sana na matakwa ya jamii- haswa jamii ya ujamaa nchini Tanzania na tena hata mazingira ya kihistoria, yaani kukua kwa miji katika Afrika na uhamaji wa watu wengi kwenye miji, hivyo kuzuka kwa utamaduni mpya mjini. Haya mazingira yalikuwa sawa na yale ambayo yalizuka mnamo karne kumi na nane kule Ulaya na yaliyozaa huo mwenendo wa Elimu Kuu"

Kutokana na nukuu hizi ni bayana kuwa Shaaban Robert ameathiriwa pakubwa na kuwaaathiri vilevile waandishi waliomtangulia na wa wakati wake, katika uandishi wa kibunilizi.

## 2.8 KIMALIZIO

Shaaban Robert kama msanii na Mwanajamii ameathirika na mambo kadha wa kadha katika uandishi wake.

Maudhui yake ameyachota katika mazingira yake na mtagusano wake wa waandishi waliomtangulia ukiwemo pia utamaduni, ukoloni, dini na tajriba yake katika maisha.

Shaaban Robert hasa alikuwa mshairi wa kutajika katika wakati wake, na katika tenzi zake zilisheheni maudhui mengi yaliyojikita katika dini hasa ya Kiislamu.

Kando na kuwa mshairi maarufu Shaaban Robert alidhihirisha umahiri wake katika kazi za nathari. Jukumu kubwa la mwanafasihi katika jamii ni kuhamasisha, kukosoa, kuelekeza, kuburudisha na kadhalika. Shaaban Robert akiwa mmojawapo wa waandishi waanzilishi wa kazi za kinathari ametalii mambo kadha wa kadha katika kazi zake za kinathari kama vile uongozi na uadilifu katika *Adili na* Nduguze (1951). Ujenzi wa jamii mpya katika *Siku ya Watenzi Wote* (1968), utu na utenda kazi bora katika *Utubora Mkulima* (1968), umuhimu wa usawa wa kijinsia katika *wasifu wa Siti Binti Saad* (1958) na mada nyinginezo katika kazi za kinathari kama vile *Kusadikika* (1948), *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1946), *Kufikirika* (1960-1961) na *Kielezo cha Insha (1951).*

# SURA YA TATU

# MTANGUSANO KATI YA FASIHI SIMULIZI NA FASIHI ANDISHI

## 3.0. UTANGULIZI

Chambilecho Mulila.A.K (2005) katika tasnifu yake ya uzamili, Mtagusano wa matini ni ugiligili unaopatikana baina ya tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiswahili unaosababisha ugumu katika kutofautisha au kutenganisha tanzu hizi mbili za Fasihi Simulizi na Andishi.

Kwa maoni yetu tofauti kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi ni ndogo sana kwani tanzu hizi mbili zinakamilishana kimaudhui, kimuundo na fani zingine kwa kiasi kikubwa.

## 3.1 MWINGILIANO MATINI KATI YA FASIHI SIMULIZI NA FASIHI ANDISHI

Ingawa sifa ya mwingiliano matini inahusishwa na nadharia za kisasa za fasihi, sifa za kuingiliana matini ina historia ndefu katika fasihi hasa tukilinganisha Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi.

Kulingana na Mulila A.K. (2005) Swahili Literature "Dhana ya Mwingiliano Matini hurejelea uhusiano kati ya matini husika na nyingine za aina yake ambazo msomaji/mwandishi amekumbana nazo.

Akimnukuu Brown na Yule (1983), anasema kuwa "Msomaji anatarajia matini aliyoisoma ilingane na ile/zile za awali katika sifa kama vile muundo, hili ni zao la mwingiliano matini na

huchukua sifa za matini nyingine tangulizi licha ya kuwa na upekee wake. Matini za aina moja huwa na sifa bia ambazo zitajibainisha, ingawa matini hizo zitazalika katika miktadha tofauti tofauti. Matini za kifasihi hutarajiwa kuwa na sifa zinazofanana licha ya kuwa fasihi ina tanzu na vitanzu mbalimbali."

Mulila A. K. katika tasnifu yake (2005), hajashughulikia wala kutoa mifano ya matini ambazo huchukua sifa sawa. Madhumuni ya utafiti wetu ni kuonyesha uhusiano huu katika matini ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

Ingawa kuna tofauti kadhaa baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi, ni muhimu kusisitiza kuwa, licha ya tofauti hizi, fasihi simulizi na fasihi andishi hutegemeana kwa mafunzo katika jamii. Ni dhahiri kuwa mchango wa fasihi simulizi katika ustawishaji wa fasihi andishi ni mkubwa mno, vivyo hivyo fasihi simulizi imefaidika kutokana na fasihi andishi katika uhifadhi wa historia za jamii mbalimbali vitabuni. Kuna mwingiliano wa sifa kati ya tanzu hizi unaokaribiana sana. Kwa hivyo, tofauti kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi ni ndogo sana.

Tunaposoma riwaya yoyote tunaziona sifa za kiutanzu zikibainika, baadhi ya riwaya katika fasihi andishi zina athari za fasihi simulizi. Kwa mfano riwaya za awali za Shaaban Robert zina athari za fasihi simulizi kama vile ufantasia. Mtindo wa usimulizi ni stadi inayotumika katika fasihi simulizi na fasihi andishi.Hususan katika fasihi simulizi, fanani mwenye uzoefu katika mbinu ya usimulizi alikuwa na ufanisi mkubwa katika kuiteka na kuinasa hadhira na kuisimulia kisa chake pasi na kuichosha hadhira yake. Shaaban Robert kama fanani katika fasihi simulizi, kwa ufundi mkubwa amekuza na kukoleza vitushi vyake barabara. Msomaji anajazwa hamu ya kutotaka

kuacha kuisoma riwaya hii kutokana na mbinu mwafaka ya taharuki. Kiu cha kutaka kujua hatima ya tukio fulani analolibuni Shaaban Robert ndicho gundi inayomnatisha msomaji katika kuendelea kusoma.

Fanani katika fasihi simulizi ndiye anayetawala hali zote katika hadithi. Kufaulu au kutofaulu kwa kisa humtegemea fanani ambaye ni msimulizi. Fanani ndiye anayeumba na kuumbua wahusika wake kwa njia ya usimulizi. Humtawala mhusika katika kila hali na uhusiano wake na mhusika ni kama wa kiumbe na Muumba. Anajua kila kitu, yuko kila mahali, anazifahamu hata fikira za wahusika wake katika hadithi.

Shaaban Robert katika *Utubora Mkulima,* amewamiliki wahusika wake kwa jinsi hii. Wahusika wake wanaeleweka kama alivyonuia waeleweke na hadhira kwa jinsi anavyowasimulia, wema wanasalia kuwa wema na wabaya kusawiriwa kuwa wabaya. Utafiti wetu umelinganisha usimulizi kama anavyosimulia Shaaban na fanani katika Fasihi Simulizi, na kuona ulinganifu mkubwa. Huenda Shaaban Robert amepata athari hizi moja kwa moja kutoka kwa hadithi alizokuwa akisimuliwa na wazazi wake kama tulivyosema katika sura ya pili ya kwamba, "Wazazi wake walimpenda na kumwamini Shaaban Robert na walimsimulia hadithi nyingi zilizoihusu jamii yake kama vile mila na desturi za ndani," ndiposa Shaaban Robert, akawaiga fanani stadi kutoka jamii yake na kuutumia ufundi huo katika uandishi wake wa riwaya y a *Utubora Mkulima*. Athari hizi na mbinu za usimulizi za Fasihi Simulizi zinahisika mwotemwote katika riwaya nzima ya *Utubora Mkulima*.

Kwa mujibu wa Mghanga (1984:4), alisaili kuwa fani tofautitofauti za fasihi simulizi kama methali, vitendawili, hadithi, nyimbo na kadhalika zilianza kuhifadhiwa katika fasihi andishi. Fasihi andishi za awali zilikaribiana sana na fasihi simulizi hasa kimuundo na kimtindo.

Ijapokuwa Mghanga anaunga mkono madai yetu kuwa fasihi simulizi imeathiri pakubwa fasihi andishi, amezingatia tu, kigezo cha umuundo na mtindo,

Fasihi Andishi imezalika kutoka kwa fasihi simulizi kwani vijitanzu vya fasihi hii vinavyopatikana katika maandiko ni vingi mno,kama vile ushairi, methali, vitendawili na kadhalika. Kwa mujibu huu basi, maoni yetu yanalingana na ya Seif Kiango katika *Ndimi Zetu* (1978), aliposema kuwa 'Imani iliyopo ni kwamba fasihi simulizi ni ghala la asilimali na amali ya uafrika wetu na kwamba ndiyo haswa chemchemi ya fasihi andishi. Hivi leo waandishi kama vile Shaaban Robert na wengine wasingefuzu kujitokeza kama waandishi wa vitabu kama si kutokana na hadithi za akina bibi...... Hadithi hizo za mabibi, siku zote zilikuwa na kusudi katika mafundisho ya maadili na elimu."

Maendeleo ya jamii iwayo ile, yamefungamana sawia na maendeleo ya fasihi. Kadri jamii inavyopiga hatua ndivyo tanzu mbalimbali za fasihi zinavyoibuka na kutiwa nguvu. Tanzu za awali kabisa katika jamii zote ni zile zinazohusiana na fasihi simulizi moja kwa moja kama ngano, mashairi, vitendawili, visaasili, methali, uigizaji na kadhalika. Tanzu hizi za kisimulizi hujidhihirisha katika fasihi andishi. Cha mno ni kuwa chimbuko la riwaya za Kiswahili ni ngano. Kwa mujibu huu, basi riwaya ya *Utubora Mkulima* ina usuli wake katika fasihi simulizi na ni kwa mantiki hii tumeshawishika kuwa riwaya hii ina athari za fasihi simulizi na kwa jumla kuwa tungo za kinathari zipatikanazo katika jamii nyingi zilikuweko kabla ya maandishi kuvumbuliwa.

Fasihi Simulizi tangu jadi imetumika kuifunza jamii mambo mengi muhimu. Maudhui ya fasihi simulizi hasa yaliangazia suala zima la maadili katika jamii na ushirikiano. Dhana ambazo ni dhahiri katika riwaya ya *Utubora Mkulima*. Wahusika Utubora, Radhia na wengine wametwikwa majukumu haya ya kuwasilisha dhana hizi na Shaaban Robert.

Maandishi ya Shaaban Robert yameshughulikia mada hasa zilizojumuishwa katika fasihi simulizi. Falsafa ya ujamaa anayoikuza Shaaban Robert katika riwaya yake ya *Utubora Mkulima* kwa kumchora mhusika Utubora, Bihaya pamoja na wengine kama wanaujamaa wanaojihusisha kwa kilimo cha kujitegemea kama vile ukulima na ufugaji kuku imetokana na athari ya fasihi simulizi ambayo ilihimiza shughuli kama vile kilimo,usasi kama baadhi ya njia za jamii kujikimu. Katika fasihi simulizi aidha, watu walijumuika pamoja wakati wa kusimuliwa hadithi, jambo ambalo lilijenga msingi imara wa ujamaa na ushirikiano katika jamii. Shaaban Robert anaangazia ushirikiano wa wanajamii kule Mrima. Hili limeafikiana na mawazo ya Senkoro F.E.M.K (2011:77) "...lengo la fasihi simulizi ni kumfanya binadamu awe mwanajamii mwema na anayeishi na wanajamii wenzake kwa mlahaka mwema. Shaaban anamsawiri mhusika Utubora kuwa kielelezo cha mwanajamii aliyeishi kwa utangamano na wenzake kule Mrima. Ukarimu, uaminifu, uhusiano baina ya Marika anaouthamini Shaaban Robert ni baadhi ya maudhui na dhamira zilizopatikana katika Fasihi Simulizi za Kiafrika.

## 3.2. HISTORIA NA MAZINGIRA

Fasihi ya Kiswahili siku zote hutumua mazingira na matukio ya historia katika umbuji wa vitushi vyake. Mazingira ya mwandishi ndimo anamochota wahusika wake na kuyatumia matukio hayo katika maisha ya kila siku kama dhamira yake kwa hadhira lengwa.

Katika Fasihi Simulizi, wanyama, mazimwi, majini, watu na vinginevyo walitumika kama wahusika na maswala yaliomulikwa katika ngano yalikuwa maadili, bidii, ukweli, utangamano, uwajibikaji, umajumui, ujima na kadhalika.

Kabla ya kuja kwa wakoloni, ngano, ngoma, vitendawili, methali ama kwa ujumla mfumo wa uzalishaji ulikuwa wa kiujima na mahusiano ya kiumajumui. Kama ilivyokuwa katika Fasihi Simulizi, Shaaban Robert ameathiriwa katika uandishi wake na mapambano yaliyokuwepo kati ya wenye ardhi na wasio na ardhi, matajiri na maskini. Mfumo huu wa ujima na umajumui anauthamini Shaaban Robert kwa kuhimiza maadili mema, ujamaa, heshima, bidii na mengineyo kwa kuwatumia wahusika wake.

Vita Vikuu vya Pili, ukoloni, kukua kwa miji kama vile Unguja ni baadhi ya mambo ya wakati wa Shaaban Robert aliyoyatumia katika kuendeleza vitushi vyake. Mhusika Utubora anaamua kuiacha kazi ya ukarani kwa Bwana Ahmed huko Unguja na kurudi Mrima baada ya kushiriki Vita vikuu vya Pili, anaamua kuuhama mji wa Unguja kwa kuchelea kunaswa katika anasa nyingi za mjini na kuhamia mashambani Mrima kinyume kabisa na ushauri wa kijakazi wake Bihaya. Mazingira ya anasa katika mji wa Unguja labda ndio sababu ya Utubora kuhamia mashambani Mrima.

### 3.3. WAHUSIKA

Kulingana na Senkoro F.E.M.K (2011:7), anasema wahusika ni watu ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe dhana au tabia za watu katika kazi ya fasihi.

Wamitila K.W (2003:123), Anasema mhusika ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya fasihi, na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Wahusika hawa wanaweza kuwa viumbe kama vile watu, wanyama, wadudu au ndege. Wahusika ndio huendeleza kazi ya fasihi; Kwa hivyo wana majukumu maalum wanayoyatekeleza. Maoni yetu ni kuwa wahusika katika kazi ya fasihi ni vyombo tu vinavyotumiwa na wasanii kufikia malengo yao katika fasihi. Jukumu la wahusika katika kazi ya fasihi ni kuwakilisha mawazo ya mwandishi na kufafanua mafunzo anayokusudia kwa hadhira yake lengwa.

Tunakubaliana naye Wamitila kuhusu athari za fasihi simulizi katika uandishi wa Shaaban Robert anaposema (2008:162) kuwa, katika historia na ukuzaji wa fasihi wahusika wanaopatikana katika kazi za mwanzoni wanafungamana na wahusika wanaopatikana katika fasihi simulizi na wanaonyesha jinsi wakati unavyoweza kuathiri mtazamo wa wahusika wa kifasihi. Kazi za shaaban zikiwa miongoni mwa kazi za mwanzoni za fasihi ya Kiswahili hasa *Utubora Mkulima* zinazo athari nyingi za fasihi simulizi.

Somo letu linaafikianana kauli ya Senkoro F.E.M.K (2011:77) ya kwamba "Mara kwa mara wahusika wa Fasihi Simulizi wanawakilisha pande kuu mbili: upande wa wema na upande wa uovu, upande wa haki na upande wa uonevu. Labda ni katika misingi hii ndimo ambamo hata baadhi ya waandishi wa fasihi ya Kiswahili wameathiriwa katika uundaji wao wa wahusika, sifa na majina ya wahusika wao hubaki kuwa ile ile tangu mwanzo hadi mwisho."

Shaaban Robert anawamudu wahusika wake kwa malengo maalum, hasa katika kudhibitisha msimamo wake kuhusu maisha kwa jumla. Mbatiah katika tasnifu yake (1990:42) kuhusu

uchambuzi wa kazi za awali za mwandishi Shaaban Robert, alisema kuwa "Hivi ni kwa sababu mwandishi huyu huwatumia sana wahusika kama makaragosi na kuwasilishia mahubiri yake."

Ni bayana kuwa Shaaban Robert anawatumia wahusika kwa kuwatawala kimawazo, kimatendo na kuenezea falsafa yake kwa njia ya mahubiri.

Athari za fasihi simulizi zinaonekana katika uandishi wa Shaaban Robert kutokana na ukweli kuwa, baadhi ya sifa za ngano ni kuwa na wahusika bapa na vilevile fanani huwatawala wahusika na vitendo vingine vyote hadithini. Utubora ni mhusika bapa na katika riwaya ya *Utubora Mkulima*, Shaaban alimtawala mhusika huyu kwa njia ya masimulizi katika matukio yake yote.

Ngano huwachukua wahusika wake katika kiwango cha jumla cha kuwakilisha tabia na matendo. Mara nyingi wahusika wa sampuli hii hutokana na jadi ya kimaadili iliyozoeleka katika ngano, hugawanywa katika mafungu mawili: wema na wabaya.

Senkoro F.E.M.K (2011:9), alisema "Wahusika wengi wa kazi za Shaaban Robert, hasa katika riwaya zake ni wahusika bapa kutokana na uhusika wao wa kingano uwafanyao wawe wema hivyo hivyo tangu mwanzo hadi mwisho na wabaya wabaki kuwa wabaya tangu mwanzo hadi mwisho."

Ingawa Shaaban Robert ametumia mtindo katika riwaya ya *Utubora Mkulima* na kujenga matukio yake yote katika misingi ya uhalisia wa maisha, ni nadra au hata haiwezekani kabisa kumpata mhusika aliyekamilika katika wema au ubaya

Matumizi ya majina katika fasihi simulizi yaliashiria tabia au sifa fulani na yalikuwa kielelezo chenye maana ya undani katika jamii ambamo majina hayo yalitumika. Shaaban Robert ameitumia mbinu hii kwa ukamilifu na ufundi mkubwa katika kuwapa wahusika wake majina ambayo yaliangazia tabia na msimamo wao tangu hapo awali. Majina kama vile Utubora na Radhia yanamwaashiria msomaji kuhusu tabia zao za wema ilhali Makuu linaashiria majivuno.

Ingawa mtindo huu unatokana na athari za fasihi simulizi inamnyima msomaji hamu na mshawasho wa kutaka kugundua tabia za wahusika. Shaaban hakuathiriwa na mtindo huu wa fasihi simulizi katika wahusika tu, bali hata majina ya mahali kama vile Busutamu.

Wahusika wenye sifa nzuri walitumika kama vielelezo kwa jamii. Wenye sifa nzuri walipaswa kuigwa na jamii ilhali wabaya walipaswa kupuuzwa.

Lengo kuu la Shaaban Robert la kutumia mtindo wa majina ya mafumbo na kutoa mukhtasari wa wasifu wa wahusika wake ni kumwongoza msomaji kuangazia jina na kujua tabia ya mhusika mwenyewe. Kugawa wahusika wake katika makundi mawili ya wema na waovu ni uelewa wake kwamba maisha ya binadamu yamegawanyika sehemu mbili: wema na uovu. Dhana inayotokana na athari za kidini. Ukweli ni kuwa maisha ya binadamu halisi ina mchanganyiko wa hali hizi

mbili kasha binadamu hujulikana kwa hali inayoizidi nyingine ikiwa ni wema, ataitwa mwema au mwovu ikiwa uovu utazidi wema.

Shaaban Robert anawasawiri wahusika wake kulingina na falsafa yake kuhusu maisha. Dhana hii ya wema na uovu ina mizizi yake katika Fasihi Simulizi, kama anavyosema Senkoro (2011:58), "Aghalabu kutokana na jadi ya kimaadili, wahusika hugawanywa katika mafungu makuu mawili: wahusika wema na wahusika wabaya.

Kulingana na Senkoro F.E.M.K (2011:75), alisema kuwa "Wako wahusika pia ambao hutumiwa kuwakilisha pande kuu mbili zinazovutana daima katika ulimwengu wa Fasihi Simulizi. Upande wa wema na haki mara kwa mara huwashinda wahusika wabaya wenye dhuluma. Kwa upande mwingine, kuna matumizi ya wahusika wasio miili, madubwana wa ajabu-ajabu, mashetani, na pia majini katika fasihi simulizi.

Vipengele hivi vya Fasihi Simulizi vimechukua sehemu kubwa katika uandishi wa riwaya ya *Utubora Mkulima* hasa katika uundaji na utumiaji wa wahusika.

Utafiti wetu wa athari za fasihi simulizi katika uandishi wa Shaaban Robert katika riwaya yake ya Utubora Mkulima, umedhihirisha wazi kuwa namna anavyounda na kuwatumia wahusika wake kuna misingi yake katika fasihi simulizi. Vilevile tunakubaliana na mawazo ya Senkoro kikamilifu kuwa:

Kwa mukhtasari, msomaji wa fasihi anatarajiwa kuwachukulia wahusika katika kazi yoyote ya fasihi kuwa tamathali fiche zinazotokana na matukio aliyoyapitia mwandishi hapo awali:

Wahusika ni mizani ya kupimia mawazo na mtazamo wa mwandishi. Mtunzi ataonyesha utu wake, mambo anayoyapenda na mambo anayoyachukia kupitia kwa wahusika katika vitushi.Hivyo basi ili kuutathmini mtazamo na msimamo wa Shaaban Robert kuhusu maisha ni lazima tutathmini namna alivyowasawiri wahusika wake.

## 3.4. TAMATHALI ZA USEMI

Mwandishi akitumia tamathali ya usemi kwa njia mwafaka, ujumbe unaokusudiwa unaweza kupokelewa na hadhira lengwa kwa njia iliyo wazi zaidi na kamilifu. Vilevile matumizi bora ya tamathali hudhihirisha tajriba ya msanii katika usanii. Matumizi bora ya tamathali za usemi huboresha mawasiliano kuhusu jambo fulani na huchochea hisia na mhemko katika uwasilishaji wa mwandishi.

TUKI (2004:393), Tamathali ya usemi ni usemi wa kufananisha dhana moja na nyingine tofauti au zinazofanana.

Naye Mbatiah (2001:77), alieleza tamathali ya usemi kama ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana na mpangilio wa maneno ili kuleta maana mpya au msisitizo.

Kama anavyosema Senkoro (1982:13), tamathali za usemi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti katika maandishi ama kusema. Hizi, wakati mwingine hutumiwa kwa njia ya kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza mvuto wa lugha.

Wataalamu hawa wote wanakubaliana kwamba tamathali ni usemi wa kufananisha kitu kimoja na kingine ili kuzua maana fiche. Hata hivyo, katika utafiti wetu tumechukua ufafanuzi wa Senkoro kama unaotufaa zaidi katika uhakiki wetu.

Baadhi ya tamathali ambazo tumefafanua katika riwaya ya *Utubora Mkulima* ni chuku, methali, taswira sadfa, nahau, tashbihi, takriri, njozi, balagha, kinaya, sitiari, taharuki, majazi na ritifaa. Ingawaje tamathali za usemi hutumika katika Fasihi Andishi na Fasihi Simulizi ni bayana kuwa zile ambazo zimetumika katika *Utubora Mkulima* zinatokana moja kwa moja na mazingira yake zinaelekea na kuhisika kama zile ambazo zingetumika iwapo kisa hiki cha *Utubora Mkulima* kilikuwa kikisimuliwa kwa hadhira na fanani hodari.

Kazi yake haidhihirishi tamathali ambazo zimeathiriwa na utamaduni wa kimagharibi kama baadhi ambazo hupatikana katika Fasihi Andishi kwa hivyo ni bayana kuwa mbinu hizi za fasihi zilishawishiwa na athari za Fasihi Simulizi.

### 3.5 CHUKU

Kulingana na Kimani na Chimerah (1999:91), chuku ni lugha ya kutilia chumvi katika kuelezea jambo ili kulipa uzito. Lengo la kufanya hivi ni kuzua picha kubwa kuhusu jambo linalosimuliwa akilini mwa hadhira, ili wasisahau haraka jambo linalozungumziwa.

Maelezo ya Mbatiah (2001:6) pia yanaoana na yale ya Kimani na Chimerah (1999) anaposema, "chuku ni tamathali ya usemi inayotumia lugha ya kutilia chumvi, aghalabu kwa madhumuni ya kusisitiza." Fafanuzi hizi zote ni muhimu kwa utafiti wetu.

Sisi tumefafanua chuku kuwa ni tamathali ya usemi inayotumia maneno ya kutilia mkazo kuhusu jambo fulani, ili kunasa makini ya hadhira na kudhihirisha uzito uliopo kuhusu jambo linaloangaziwa.

Katika utafiti wetu, tumebainisha na kutathmini matumizi ya chuku katika riwaya ya *Utubora Mkulima*. Baadhi ya matumizi ya chuku ni katika Uk 1, pale Shaaban Robert anamwelezea mhusika wake Utubora kuwa, kwa kushika majira alikuwa kama saa. Kazini alikuwa wa kwanza kufika na wa mwisho kutoka.

Kwa matendo haya ya sifa, "Utubora alikuwa kama pumzi ya maisha kwa tajiri wake ambaye alikuwa hana mtu mwingine bora wa kumtegemea".

Vilevile Shaaban Robert ametilia chumvi anapomsawiri Utubora kuwa mkarimu kiasi cha kuweza kuingia katika kiunga cha Bimkubwa bila idhini yake na kuanza kukinadhifisha

kiunga chake. Mwandishi anaeleza (1968:9) kwa kuwa miguu yake mtu humwongoza kwenye neno lililo katika moyo wake, siku moja asubuhi Utubora aliamka mapema kabisa. Akachukua mundu wake akashika njia ya kwenda kwa Bimkubwa yule aliyekuwa hataki kuonana na watu. Baada ya mwendo wa dakika chache alijiona amesimama katika uwanja uliorufukiwa. Alichagua kuanza kazi yake katika upande wa mbele.

Kutokana na maelezo haya, mwandishi anataka tumwone Utubora kuwa mtu mwema kupita kiasi, hali ambayo ni ngumu kwa mwanadamu kwani hakuna binadamu mkamilifu.

## 3.6 NAHAU

Nahau ni vifungu vya maneno vyenye maana fiche. Maana hii haitokani na maneno yanayopatikana katika nahau. Hivyo basi, inambidi msomaji wa kazi ya fasihi kutafakari maana anayokusudia mwandishi katika nahau iliyotumika. Chambilecho Wamitila (2003:163), nahau huwa na undani wa maana kuliko baadhi ya misemo inayopatikana katika lugha fulani. Kimuundo nahau huwa na kitenzi na nomino.

Shaaban Robert katika riwaya yake ya *Utubora Mkulima* ametumia baadhi ya nahau kama zifuatazo:

Uk 50...mapenzi yalimsaliti: Baada ya uchumba wa Utubora na Sheha kuvunjika, Utubora aliona mapenzi yamemdhalilisha na kuahidi kuepuka kabisa swala la mapenzi maishani mwake.

Uk 70...Hata bughudhi sura: Radhia alidhani kuwa hali ya uchochole ya Utubora itamkirihi mamake, lakini umbo lake lilivutia na halikumkasirisha mama jambo ambalo lilimridhishaRadhia.

Uk 68...Kubadili hewa – kuhama kutoka jijini Unguja na kuelekea mashambani Mrima ilikuwa ni kuanza kuishi maisha tofauti na yenye utulivu kinyume na ilivyokuwa kule mjini Unguja.

## 3.7. TASHBIHI

Beckson na Arthur (1969:203), wanaeleza, kwamba tashbihi ni usemi unaolinganisha vitu viwili vilivyofanana kwa kutumia maneno: 'kama' 'au' 'sawa na' mithili ya' 'ja' na kadhalika. Korg (1959:8), anatoa mawazo sawa na haya. Anasema kwamba tashbihi ni tamathali ya usemi inayotumia maneno kama: 'sawa na' kuonyesha kuwa ulinganishi unafanywa.

Tathmini ya maelezo haya yote inaonyesha kwamba wataalamu hawa wote wanaelezea maana ya tashbihi kwa njia sawa. Ni usemi wa kufananisha.

Picha inayochorwa na mwandishi anapotumia mbinu hii huwa na athari kubwa kwa hadhira. Katika utafiti wetu tumechunguza jinsi Shaaban Robert alivyotumia mbinu hii ya tashbihi na kuonyesha baadhi ya tashbihi hizo.

Uk 12: Alijiona kuwa kama mfungwa pale. Utubora analinganishwa na mfungwa kazini kwa Ahmed. Kazi hii ilimnyima nafasi ya starehe.

Uk 13: Mrima mimi na wewe tukae kama Adamu alivyoishi, kwa kazi ya mikono na jasho la vipaji vyetu wenyewe. Shaaban anatumia tashbihi hii kwa kuienzi kazi ya ukulima, kazi aliyoamriwa Adamu na Muumba.

Uk 15: Bihaya alikunja kipaji chake na kuwa na makunyugu kama ngozi ya kifaru. Bihaya alikasirishwa sana na wazo la Utubora kuacha kazi kwa Ahmed.

Uk 43: Kijana huyu alikuwa kama mboni ya jicho kwa bibi yake. Umuhimu wa mjukuu aliyekufa vitani unadhihirishwa na tashbihi hii. Alikuwa wa kutegemewa kama ilivyo mboni kwa uwezo wa kuona.

Uk 63: Kutafuta furaha katika maisha ni kama kutafuta paka mweusi katika chumba cha giza. Tashbihi hii inatilia mkazo falsafa ya kidini yake Shaaban kuhusu maisha kuwa furaha hupatikana akhera si duniani.

Uk 74: Radhia alikuwa kwa Utubora kama hewa nzuri ya asubuhi, na sauti yake changa ilikuwa kama kinanda katika masikio yake. Mfano wa waridi uenezao uzuri na furaha pande zote...Shaaban katika kumfanya Radhia kuonekana wa kuridhisha kama jina alilompa anatumia kila aina ya ulinganishi mzuri ili kuafikia kusudi lake la kutaka aigwe na hadhira yake.

Uk 84: Sheha aliposoma barua hii alikasirika sana. Aliona kuwa habari zote zilikuwa kama hekaya katika hadithi za Abunuwasi. Shaaban anabainisha matumaini aliyokuwa nayo Sheha ya kuolewa na Utubora baada ya kutalakiwa na mme wake.

Umaarufu wa Shaaban Robert katika matumizi ya tashbihi umemwezesha kuyafanya mawazo yake yaguse zaidi kutokana na matumizi mema ya tashbihi kama ilivyodhihirika hapo juu.

## 3.8 KINAYA

Kinaya huweza kutumiwa kama njia ya kuonyesha upungufu fulani wa mhusika hasa kuhusiana na suala fulani.Kinaya huchangia kwa kiasi Fulani kuonyesha udhaifu wa kibinadamu.

Msokile M. (1993:83), anaeleza kinaya kuwa ni tamathali ya usemi yenye maana kinyume na kile kinachosemwa.

Naye Mbatiah (2001:32), anaafikiana na Msokile lakini anaongeza kuwa kinaya ni usemi wenye maana iliyo kinyume na kile kinachosemwa. Anasema kuwa kinaya cha: jaala, kihali, usemi na dhihaka, kinaya cha usemi, ni kauli ambayo inasema jambo lililo kinyume na kile msemaji anachomaanisha.

Wamitila (2008:411), anasema kwamba kinaya cha dhihaka hurejelea hali ambapo mbali na kumaanisha kinyume na jambo lililosemwa pia, hukusudia kukera, kuudhi au kumletea mlengwa hisia za kudharauliwa.

Senkoro (1982:20), anasema kuwa aina hii ya kinaya ina ubeuzi mkali na jahili unaopenya kweli.

Kuhenga (1977:71), anafafanua kinaya kama usemi wa mafumbo, ambao kwa msemaji kwa maneno yake ya kebehi ya kisirisiri, hutoa wasifu kwa matendo yasiyofaa, ilhali moyoni mwake anakusudia kinyume cha matamko yake.

Fafanuzi yetu kwa mukhtasari ni kuwa, kinaya ni tamathali ya usemi inayoelezea maana kinyume na kinachosemwa ili kufikia lengo fulani.

Katika utafiti wetu, fasiri ya, Kuhenga itatufaa sana katika kubainisha kejeli katika kazi ya Shaaban Robert 'Utubora Mkulima'.

Mamake Radhia alimuelezea Dharia Uk 66….lakini sioni kama naweza kumkaribisha mkulima hapa. Pana mipaka ya kutenda kila neno hata katika siku hizi za uhuru. Fahamu kuwa uhuru ni dhima ilazimishayo adabu na heshima: ustahiki na adili na mengine mengi kama hayo juu ya mtu. Haya ni maneno ya mamaye Radhia, heshima na adabu, ustahiki na adili anazozungumzia yeye binafsi hanazo kwani anaona ni fedheha kumkaribisha mkulima ambaye ni wa tabaka la chini nyumbani kwake. Shaaban anatuonyesha jinsi enzi hizo ukulima ulidharauliwa ilhali ulikuwa ndio msingi wa maendeleo ya taifa lolote na hasa ni kazi aliyopewa mwanadamu kutoka kwa Muumba.

Uk 68 "….labda hiyo ndiyo sababu nilimkubali Makuu!" Kinaya hiki kimetumiwa kimakusudi na Shaaban Robert kupinga kuwa Radhia ambaye Shaaban anamchora kama mhusika mwema, asingepotoshwa na utajiri alioukashifu mwandishi na kuolewa na tajiri Makuu. Hivyo basi Radhia anakana kuwa si sababu ya mali itakayomfanya aolewe na Makuu ambaye amesawiriwa kama mtu wa majivuno au makuu. Hii inatuwekea wazi falsafa ya Shaaban kuhusu fedha kuwa si kila kitu maishani."Kando na kuwa na pesa, binadamu anahitaji kuwa na utu.

UK 72 "...sidhani kuwa hilo litamdhuru mtu yeyote isipokuwa wewe mwenyewe. Ukitaka kweli si haki yako kujifanya kuwa hudhuriwi na maangamizi ya ulimwengu." Tayari Sheha alikuwa amedhuriwa kwa kutalakiwa na mumewe aliyekuwa tajiri, vilevile kwenda kwa Sheha kwake Utubora kulionekana kumdhuru mchumba mtarajia Radhia. Hivyo basi mawazo haya ya Radhia kwa binamuye Sheha ni kinaya tupu. Kila mmoja wao anammezea mate Utubora huku akikana hali hii.

Uk 85: Sheha alinena, "Pole Utubora! Lakini mabadiliko ndiyo desturi ya wagonjwa." Pole anayompa Utubora kwa kuikosa kazi kwa Bwana Ahmed ni kinaya, kwani ilikuwa njama yake na shangazi yake ili Utubora asiipate kazi hii na kumuoa Radhia.

## 3.9 TAHARUKI

Kulingana na Wamitila (2003:212), Istilahi hii hutumiwa kuelezea hamu anayokuwa nayo msomaji kutaka kujua yatakayotokea katika hadithi fulani..."

Kulingana na Senkoro (2011:51), ' ...Taharuki ni hali ya kusisimshwa kwa hadhira kutokana na shauku ya kutaka kujua jinsi mambo yatakavyojiri katika sura ama sehemu zijazo za kazi ya fasihi...'

Fasiri yetu ni kuwa taharuki ni mbinu ya mwaandishi kumficha au kuhairisha matokeo ya tukio fulani kwa kumtaka msomaji au msikilizaji kuendelea kusoma au kusikiliza.

Katika riwaya ya *Utubora mkulima* tunapata matumizi ya mbinu hii pale ambapo Utubora anaandika barua akiomba idhini ya kukinadhifisha kiunga cha Bimkubwa.Utubora anasubiri majibu kwa hamu lakini hayaji.Kisha anamua kuifanya kazi hiyo bila kupata idhini.Wakati akiendelea kufanya kazi ya kukata magugu ambapo alipuuzwa kabisa na Bimkubwa, msomaji anaingiwa na hamu ya kutaka kujua kutatokea nini hatimaye.

Vilevile taharuki inajitokeza pale ambapo Radhia amevunja uchumba wake na Makuu.Utubora aliamua kusafiri kuondoka Busutamu ili kuuondoa uwezekano wa uchumba kati ya Makuu na Radhia kuvurugika ikiwa angeendelea kubakia Busutamu .Msomaji anakuwa na hamu ya kuendelea kusoma ili ajue hatima ya uchumba kati ya Makuuna Radhia utakavyokuwa.

Tanzu mbalimbali za fasihi simulizi hutumia taharuki ili kuvuta usikivu wa hadhira.Hadhira hujiuliza mara kwa mara kuhusu matukio yatakayofuatia kuwa yatakuwa ya namna gani.Taharuki inaweza kutumiwa si kwa yale yanayoelrzwa tu, bali pia jinsi yanavyotolewa na mtambaji

## 3.10. **SADFA.**

Wamitila (2003:186), Hii ni dhana inayotumiwa katika fasihi simulizi kuelezea utukiaji wa matukio kwa wakati mmoja na aghalabu kwa namna inayoshangaza au inayoashiria bahati..."

Sadfa ni matukio mawili au zaidi yanayotokea katika hadithi kana kwamba yalipangwa na yana uhusiano mkubwa kisababishi. Shaaban Robert ameitumia mbinu hii pale ambapo Utubora na

Radhia wanafunga ndoa lakini hawana mali yoyote inasadifu kuwa ni wakati huu ambapo Bimkubwa anaaga dunia na kumwachia Utubora urathi wake wote.

## 3.11. MBINU YA MAJAZI

Hii ni mbinu ya kutumia majina ambayo yanafumbata tabia, sifa au matendo ya wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi. Mbinu hii inamrahisishia msomaji kazi ya kuwaelewa wahusika au sifa za mahali katika kazi ya kifasihi.

Mbinu hii ni aina ya upenyezi hasa kwa kuliteua na kulitumia jina fulani mwandishi anamwelekeza msomaji kwenye tathmini au uelewaji fulani mahususi. Shaaaban Robert katika riwaya ya *Utubora Mkulima*, ametumia majina kama vile:

**UTUBORA** –kwa maana ya mtu mwenye utu ambaye anashiriki kazi ya ukulima kinyume na Makuu ambaye alikuwa na majivuno kwa sababu ya mali mhusika Utubora alikuwa na utu.

**RADHIA**-kitabia na kimaumbile mhusika Radhia alikuwa anaridhirisha ambapo ni kinyume na mhusika Sheha ambaye alivunja uchumba wake na Utubora na baadaye kumfanyia njama asipate kazi katika kampuni ya babake.

**MAKUU**- Makuu alijiona bora kutokana na uwezo wake wa kiuchumi na hivyo kukosa thamana kwa waliokuwa maskini ilhali wote wameumbwa na Mola.

## 3.12 RITIFAA

Hii ni tamathali ambapo kitu kisichokuwa na uhai huzungumziwa kama kilicho na uhai au mtu ambaye yupo na anasikiliza maneno yanayosemwa.Mfano ni pale utubora anapozungumza na marehemu mamaye kana kwamba yu hai na wapo pamoja.

Mbinu hii ya lugha iltumika katika jamii za kale na hata sasa wakati ambapo mtu ameaga,watu huomboleza wakimwita na kuongea naye kana kwamba anasikia.

Mfano mzuri ni katika uk.30 'Mama najua kuwa upo hapa ingawa sina macho ya kukuona..."Utubora alimsemesha marehemu mamayake

## 3.13 KIMALIZIO

Tumepambuanua mwingiliano matini kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi.

Katika utafiti wetu mtagusano huu umejikita katika baadhi ya vipengele vya fasihi ya Kiswahili kama vile wahusika na pia historia na mazingira katika tanzu hizi mbili.Matokeo ni kuwa,tofauti iliyopo kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi ni ndogo sana kaisi cha kutobainika kwa urahisi ,kwani tanzu hizi mbili zinachangiana kwa kiasi kikubwa kifani na kimuundo.Vilevile katika sura hii tumeweza kushughulikia baadhi ya tamathali za usemi tukijikita na kutoa mifano mwafaka kutoka kwa riwaya ya *Utubora Mkulima.*

Tamathali tulizozishughulikia ni zile tulizoona zinafaa zaidi katika utafiti wetu kama vile chuku, nahau, tashbih,i kinaya, taharuki na sadfa.Tamathali hizi ni baadhi tu ya zinazotumika sana katika fasihi simulizi na vilevile zinatumika katika fasihi andishi katika kuyafanya maandishi yavutie kwa msomaji.

## SURA YA NNE

## USIMULIZI KATIKA RIWAYA YA UTUBORA MKULIMA

### 4.0. UTANGULIZI

Usimulizi ni wakala nyenzo, mbinu au njia inayotumiwa na mwandishi kuisimulia hadithi au kisa chake.swala la usimulizi limefafanuliwa na wataalamu mbalimbali wakiwemo; Wamitila, Madumula na wengineo.

Kulingana na Wamitila (2003:325), usimulizi ni uelezaji wa matukio katika hadithi Njogu K. na Chimerah R. (1999), wanafafanua usimulizi kama sauti ya uwasilishaji wa hadithi na hivyo kudai kuwa kuna aina mbili za usimulizi. Usimulizi wa mwandishi mwenyewe anapotumia nafsi ya tatu na usimulizi ambapo mmoja wa wahusika anasimulia hadithi.

Madumulla J. S. (2009:110), anasema kwamba "usimuliaji ni mbinu katika fasihi inayobainisha sehemu alipo anayesimulia hadithi au tukio. Kwa jinsi hiyo, msemaji anapata picha ya jinsi matukio yanavyohusiana, yanavyosababishana na yanavyoendelea kutoka mwanzo hadi mwisho.

Pamoja na kwamba usimulizi ni kurunzi ya kumtafutia mwandishi alipo kama anavyotueleza Madumulla, haja na msingi wa utafiti wetu ni athari za usimulizi huu katika riwaya ya *Utubora Mkulima* kwa msomaji au hadhira.

Kwa maoni yetu, masimulizi yanachangia uelewa na umaizi wa kazi ya fasihi, kwani usimulizi mzuri humfanya msomaji kufuatilia na kuyaelewa yanayosimuliwa bila kutatizika.

Fasiri yetu ni kuwa usimulizi ni namna hadithi inavyowasilishwa kwa hadhira na msanii na nafasi anayoichukua katika hadithi yenyewe.Ni njia kuu ya mtunzi wa riwaya ya kudhibiti na kujenga maudhui yake.usimuliaji huelekeza ujenzi wa wahusika,matukio na kila kinachowasilishwa katika riwaya .

Kwa msomaji usimulizi hudhibiti hisia zake juu ya yote ayasemayo. Usimuliaji hufanya tuone, tusikie, tunuse na hata kuonja hadithi ilio katika maandishi tu.Hutufanya tupate hamu au matamanio, woga na kuchukua msimamo kutokana na yale tulioyasoma. Hadithi yoyote ile husimuliwa na msimulizi ambaye anaweza kushiriki katika matukio anayoyasimulia yeye mwenyewe, kupitia kwa wahusika wake au kutoshiriki kabisa.

Ili kuelewa usimulizi katika kazi ya fasihi maswali kama vile je,usimulizi wa hadithi unafululiza au una mikato isiyokuwa ya kawaida?,Je,usimulizi huu ni wa aina gani?Je, ni usimulizi wa moja kwa moja au ni usimulizi changamano?Je,ni usimulizi wa nafsi ya kwanza, ya pili, nafsi ya tatu au mchanganyiko wa nafsi ya kwanza na tatu?Je,usimulizi huo unafungamana kwa kiasi gani na masuala yanayozungumziwa katika kazi hiyo?Je, usimulizi huo unaonyesha ubunifu wa aina yoyote au unatumia mbinu ya fasihi simulizi?Je, mitindo inaoyoonekana ina athari gani katika uelewaji wa kazi inayohusika?

## 4.1 AINA ZA USIMULIZI

Kulingana na Wamitila (2008), waandishi werngi wa kazi za kubuni wana mazoea ya kuandika kazi zao kwa kutumia usimulizi wa nafsi ya kwanza na ya tatu. Hata hivyo kuna baadhi ya

waandishi wengine anbao walitumia nafsi ya pili kama vile Michael Butor aliitumia nafsi ya pili katika riwaya yake ya *Second Thoughts* ( 1957).

Ingawa katika utafiti wetu tuliona maoni haya kuwa muhimu, Rodger Fowler katika nukuu hii, hajaangazia kuwa upendeleo na uzoefu wa mwandishi ni muhimu katika kuchagua nafsi atakayoitumia. Usimulizi anaoutumia mwandishi kimsingi huwa ni chaguo lake ambalo hutokana na tajiriba ufaafu katika kuwasilisha ujumbe wake.

Naye J.A. Cuddon katika kitabu chake '*A Dictionary of Literary Terms*' (1979:745), anaeleza kuwa: kuna namna michanganyiko mbalimbali, ijapokuwa ni aina tatu tu za msingi ambazo zinaweza kubainishwa. Kwanza ni usimuliaji maizi ...pili ni wa nafsi ya tatu...tatu ni usimuliaji wa nafsi ya kwanza...michanganyiko mbalimbali ya njia hizi imejaribiwa na watunzi wengi, mara nyingi kwa makusudi, mara nyingine, kwa mpangilio ambao si mzuri.

Jambo muhimu katika aina hizi za usimulizi kulingana na mtazamo wetu ni ujumla wa mambo mengi kutoka kwa mwandishi, hadhira lengwa na kusudi la hadithi yenyewe. Mitazamo ya usimulizi inaweza kuangaziwa kwa namna mbili kuu, mtazamo wa ndani na mtazamo wa nje. Katika mtazamo wa ndani msimulizi huwa anashiriki katika hadithi kama mhusika. Katika hali hii sauti inayosimulia inatumia nafsi ya kwanza ambapo mhusika huyu anakuwa na nafuu na uhuru wa kutofuatiliwa unyo unyo na msimulizi, hivyo basi, msomaji anamfuatilia kwa jicho la mhusika na wala si msimulizi ndani ya mhusika na kukubaliana na mtazamo wa mhusika katika masuala mbalimbali.

Mtazamo huu wa ndani unaweza kubadilikabadilika kutoka mhusika hadi mhusika, hali ambayo inatoa taswira kamili kuhusu matukio ya hadithi kwa vile inaonyeshwa jinsi wahusika tofautitofauti wanavyohakiki na kuhukumu matukio na mawazo sawa kwa njia mbalimbali.

Katika mtazamo wa nje, msimulizi katika hadithi huwa hatambuliki, kiwakilishi nafsi ya tatu 'a' ndicho hutumika. Kuna aina anuwai za mtazamo au usimulizi wa nafsi ya tatu kama vile usimulizi maizi wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi ana sifa za kiungu za kujua na kumtawala mhusika kwa kila hali. Uhusiano wa mhusika kwa msimulizi unaweza kumithilishwa na ule wa kiumbe na Muumba. Msimulizi anakuwa kila mahali kwa wakati mmoja na anajua tangu mwanzo hadi mwisho wa mambo yote katika hadithi

## 4.2. USIMULIZI WA NAFSI YA KWANZA.

Usimulizi wa nafsi ya kwanza hutokea pale ambapo msimulizi wa hadithi anajitambulisha kwa viwakilishi 'mimi'au mofu 'ni' iliyoambishwa kwenye kitenzi.Katika usimulizi wa aina hii mtazamo unaelezwa kama mtazamo wa ndani.

Msimulizi wa nafsi ya kwanza kimsingi ni yule ambaye anasimuliwa na yule anayetazama na kuyatathmini matukio yanayosimuliwa.Riwaya zinazosimuliwa kwa nafsi ya kwanza huweza kuwa na wepesi wa kutambua msimulizi wake ni nani ,kwa mfano katika riwaya ya *Siku Njema*,yake Ken Walibora tunagundua kuwa sauti ya kisimulizi ni Kongowea Mswahili ambaye ni mhusika katika riwaya hii.

Usimulizi wa nafsi ya kwanza pia unaweza kufanywa na wahusika wawili au zaidi .Katika masimulizi ya nafsi ya kwanza mhusika hutumika kama chombo.

Usimulizi wa nafsi ya kwanza hutekeleza wajibu wa kuonyesha msukumo wa matendo ya mhusika, kufichua migongano ya kiitikadi inayomjia mhusika mwenyewe kuelekeza kwenye ndoto zake na kadhalika, na huweza kuwa msingi wa kujenga uhusiano wa karibu kati ya mhusika anayehusika na msomaji kwa njia ya masafa ya ujumi.Msimulizi wa nafsi ya kwanza anaweza kuwa msimulizi mbabe,yaani yeye ndiye shujaa katika kazi anayosimulia, anaweza vilevile akawa msimulizi asiye mbabe au akawa msimulizi mshuhudiaji. Katika masimulizi ya nafsi ya kwanza,msimuliaji hujulikana kama msimuliaji *shahidi* ambaye anapenda kutumia mtindo wa kitawasifu ambao unafanya asiwe na uwezo wa kuona kila kitu bali kuwa na uwezo wa kuona na kujua mambo mahususi tu.

Mulokozi M.M(1996:33), anatumia usimulizi wa nafsi ya kwanza katika riwaya yake ya *Moto wa Mianzi,*`'kwa muda wa siku tatu tulitembea porini na kulala porini.Tulipika chakula porini na kukila huko huko porini.Usiku tulikoka moto na kuuota.Tulitandika na kulala chini ya miti au vichaka.Hutukutaka kulala vijijini kwa kuchelea kugunduliwa na Wadachi.

Siku ya kwanza tulitoka Idegesi tukapita katika mabwawa ya Luteme katika eneo la Ihemi na kusafiri usiku kucha kupitia katika nyika ya magunga kusini ya Isombe.Kutoka hapo, tukanyoosha njia kuelekea kaskazini-mashariki, hadi tulipopiga kambi kusini mwa Kipeng`elo kando kando ya mto wa Luvaha Ndogo.Nia yetu ilikuwa ni kushinda pale kambini mchana kutwa,jioni tuingie kijijini kipeng`elogizani bila kuonekana"

Matukio katika nafsi ya kwanza huenda kwa kasi kama tunavyoona katika mfano tulioutaja awali, msomaji anahisi masafa na wakati katika matukio yanavyojipambanua katika hadithi..Aidha msimulizi anayaeleza yale anayoyashuhudia. Mfano huu unashabihiana na masimulizi ya nafsi ya kwanza ya kitawasifu ya kazi ya kinathari ya Maisha *Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* ya Shaaban Robert.

## 4.3. USIMULIZI WA NAFSI YA PILI

Aina hii ya usimulizi unahusishwa na nafsi ya pili 'wewe'au mofu'u'.Usimulizi huu si wa kawaida katika kazi za kifasihi zilizoandikwa kwa Kiswahili. Baadhi ya riwaya ambazo zimetumia mtindo huu wa usimulizi ni:Dharau *ya Ini* na *Dunia Yao*.

Kazi za kifasihi tulizozitaja awali zimeishia kuchanganya nafsi katika usimulizi wao, kumaanisha kuwa usimulizi wa nafsi ya pili ni mgumu na kazi za masimulizi ya nafsi hii ni chache mno.

Shaaban Robert ameitumia nafsi hii katika riwaya yake ya *Utubora Mkulima* pale anapotumia mtindo wa mazungumzo baina ya wahusika wake wawili Sheha na Utubora( 1968:.82). Katika muktadha huuSheha alikuwa akimdadisi Utubora akinuia kugundua iwapo angalikubali kurudi kazi kwa babake, bwana Ahmed ambayo alikuwa ameiacha hapo mbeleni.

## 4.4. USIMULIZI WA NAFSI YA TATU

Uandishi wa riwaya kwa muda mrefu umetumia nafsi ya tatu katika kazi za fasihi za kinathari hasa hasa riwaya ya Utubora mkulima. Usimuliaji huu unaruhusu msimumulizi awe kila mahali anapotaka kuwa na wakati wowote katika usimulizi wake.Shaaban Robert ametumia nafsi hii ya tatu katika riwaya yake ya Kusadikika.

(1948:45-46 ), 'anapoelezakuwa baada ya wajumbe watano kufanyiza kazi zilizowaletea msiba mkubwa, mjumbe wa sita alihitajiwa kuenda katika ardhi.Ilikuwa kama kusadikika ilitaka kuwapa ujumbe watu wote utakaoishia katika kifungo, mjumbe aliyepatikana kwa safari hii, labda iliyo ya miujiza mikubwa sana kuliko zile zilizotangulia zote, alikuwa Amini. Amini alishuka katika ardhi kwa msaada uliopatikana kwa Mangera,ndege wakubwa kabisa walishao katika ardhi lakini walalao Kusadikika. Wakati wa kuenda chini, Amini alijifunga bila ya kujulikana juu ya paja la Mangera aliyekuwa amelala fofofo usiku.Kulipokucha ndege huyo aliamka akaruka mpaka chini.Akatua ziwani, nusu ya mapaja yake ilikuwa majini. Kwa hivi Amini alijifungua, akaogelea bila ya kuonekana mpaka ufukoni.ziwa hilo lilikuwa na maji baridi sana .Amini aliota jua mchana kutwa ili kuondoa msisimo wa maji hayo.Hali ilipokuwa njema tena alizizuru pande zote za ardhi kama alivyotakiwa na kazi yake.Wakati wa kurudi kusadikika mjumbe huyu alijifunga tena juu ya paja la Mangera aliyekuwa ameshughulika na karamu ya mizoga wa ndovu bila kutazama huku wala huko.safari hizi zilikuwa za ajabu na hatari kubwa kabisa.."

Kuhusu kisa hiki ingawa msomaji hamwoni msimuliaji anahisi na kuona uwezo wake kwa kufuatilia masaibu ya mhusika wake, Amini.anamfuatilia usiku akienda kujifunga kwenye paja

la Mangera na kumfuatilia Mangera mpaka ziwa la ardhi.Msimuliaji anamtawala mhusika kama chombo cha kufanyia kazi.Kuwepo kila mahali kwa wakati mmoja na kujua kila kitu ni jambo lisilowezekana kwa binadamu.Uwezo huu katika kisa hiki ni wa kufikirika tu.

Sifa mojawapo ya riwaya zinazosimuliwa katika nafsi ya tatu ni kuwa, hutumia usimulizi kihusika.katika usimulizi huu mhusika anayepatikana humo aghalabu huwa anashiriki matukio anayoyasimulia.Kimsingi mwandishi anawasiliana na hadhira yake kupitia kwa mhusika fulani ambaye anawasiliana na msimuliwa.

Usimuliaji maizi kwa kiasi kikubwa , ni matokeo ya usimulizi wa nafsi ya tatu.katika usimulizi huu,msimulizi huenda kutoka kwa mhusika mmoja hadi mwingine,sehemu moja hadi nyingine tukio hadi tukio kwa uhuru mkubwa kabisa wa kumtawala mhusika kwa namna zote atakazo.

Mbinu hii inatumika katika riwaya ya Utubora *Mkulima*, (1968:70), mwandishi anapotueleza kuhusu dhifa ilioandaliwa kwa Liwali kama ifuatavyo:

> 'Siku iliyokusudiwa kwa dhifa ilipofika Utubora alioga akavaa mavazi yake kwa uangalifu sana .Alipokwisha vaa akajitazama kiooni.bila ya kiburi chochote alisema moyoni mwake kwamba alikuwa "mrembo".Utubora alikuwa mrembo kweli kweli,kwa sababu alikuwa na umbo lililokuwa linachukuana vema na mavazi"

Katika usimulizi wa nafsi ya tatu, msimulizi katika hadithi huwa hatambuliki, kiwakilishi nafsi ya tatu 'a' ndicho hutumika. Kuna aina anuwai za mtazamo au usimulizi wa nafsi ya tatu kama vile usimulizi maizi wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi ana sifa za kiungu za kujua na kumtawala mhusika kwa kila hali. Uhusiano wa mhusika na msimulizi unaweza kumithilishwa na ule wa kiumbe na Muumba. Msimulizi anakuwa kila mahali kwa wakati mmoja na anajua tangu mwanzo hadi mwisho mambo yote katika hadithi, chambilecho Liberman, (1968:143).

> "Msimulizi anajua kila kitu kinachohitajika kujulikana
>
> kuhusu wahusika na matukio, yu huru kwenda
>
> popote kila wakati anavyotaka kutoka kwa mhusika
>
> hadi mhusika na kusema anachotaka kuhusu unenaji
>
> na vitendo vya wahusika. Ana uwezo wa kujua
>
> ndoto hisia na nia za wahusika."

Mhusika anayemwelezea Liberman, anastahili kuitwa kifaa, sababu hana aliwazalo yeye wala uhuru wa uamuzi wa kibinafsi kwani maungo na hisia zake zote zinamilikiwa na kutumiwa na msimulizi. Hali hii haiaminiki katika hali ya kawaida, kwani katika hali halisi mtu hawezi kummiliki binadamu mwenza kwa kiwango hiki. Mtazamo huu ni wa kidhahania tu.

Kulingana na Madumula J.S.(2009), Usimuliaji wa nafsi ya tatu umegawika katika usimuliaji tinde au shinda, usimuliaji horomo na usimuliaji penyezi.Shinda ukiwa ni usimuliaji usio wa

kutegemewa ilhali horomo ni usimuliaji wingi huku penyezi ukiwa usimuliaji ambapo msimulizi huingia katika nafsi ya mhusika na kujitokeza kama mhusika mwenyewe.

Katika riwaya, mambo yanayohusiana na usimulizi ni uonyeshi ambapo wahusika katika riwaya wanawasilishwa zaidi kimatendo na uelezaji ambapo msimulizi anaeleza kila kitu katika kisa.

Katika kazi ya kifasihi, matukio yanapowasilishwa katika hadithi, huwa yanawakilishwa katika mkondo fulani wa mwono ambao hutegemea mwandishi.Mkondo wenyewe waweza kuwa wa kibunilizi au kihistoria kwa nia ya kutoa picha ya kweli kuhusu matukio haya kwa makusudi mbalimbali kwa hadhira lengwa. Kila mwandishi huwa na mkabala uliotofauti wa kuwasilishia maoni, hisia, au mtazamo wake wa kituko katika uandishi.

Liberman (1968:92), anasema kuwa "Mtazamo ni msimamo wa kifalsafa wa mwandishi pamoja na upendeleo wake wa kijamii na kimawazo kuhusu matukio na wahusika katika hadithi." Ingawa ayasemayo Liberman ni kweli, lakini kama tulivyoona awali falsafa ya mwandishi ni tukio la mambo kadha wa kadha katika maisha yake. Hivyo, mtazamo wa mwandishi fulani huwa na chembechembe za athari za waandishi wa awali au wa wakati wake.

Katika utafiti wetu tumebainisha jinsi falsafa ya Shaaban Robert ilivyoathiriwa na waandishi waliomtangulia na wa wakati wake, pamoja na mazingira, dini, utamaduni, historia na kadhalika.

Hali hizi zinajidhihirisha katika usimulizi wake kwenye riwaya ya *Utubora Mkulima* kwa namna anavyotumia lugha, kuwachora wahusika wake na hata maudhui anayoyazingatia katika usimulizi wake. Mtazamo wake umeathiriwa na mambo mengi ikiwemo fasihi simulizi.

## 4.5. KIMALIZIO

Katika sura hii, tumeshughulikia hasa usimulizi na aina zake na kuonyesha namna Shaaban Robert alivyoteua aina ya usimulizi aliouatumia.Imebainika kwenye sura hii kuwa Shaaban ametumia usimulizi wa nafsi zote tatu na mifano mwafaka imetolewa.

Vilevile tumeangalia katika utafiti wetu umuhimu na athari za mbinu hii ya usimulizi kwa msomaji. Ilibainika kwamba Usimulizi wa hadithi ukiwa mbaya unaathiri uelewa wa msomaji.

Mwandishi mahiri hufanikisha kazi yake kwa kumsawiri mhusika au wahusika wake kulingana na mafunzo anayonuia kuifunza jamii au hadhira yake lengwa.

Katika utafiti huu vilevile imebainika kuwa nafsi ya kwanza na ya tatu ndizo hutumika sana katika kazi za kinathari za lugha ya Kiswahili, ingawa kuna mifano michache ya riwaya zilizoandikwa katika nafsi ya pili. Aidha matumizi ya nafsi zote tatu yamebainika katika kazi nyingi za kinathari za lugha ya Kiswahili.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0. UTANGULIZI

Kazi hii, imeshughulikia matokeo ya utafiti wetu na mikakati tuliyotumia ili kufikia maleng yetu. Utafiti wetu ulichunguza athari za Fasihi Simulizi katika uandishi wa Shaaban Rober tukijikita katika kazi yake ya riwaya *Utubora Mkulima (1968).* Ili kufafanua baadhi y vipengele vya Fasihi Simulizi vinavyojitokeza katika Fasihi Andishi tulilazimika pia kurejele vitabu vingine muafaka. Hatimaye tulitoa mapendekezo yetu ambayo tunaamini yatakuwa y manufaa kwa watafiti watakaokuja baada yetu.

## 5.1 MUHTASARI

Tulijikita katika riwaya ya *Utubora Mkulima* na kuonyesha athari za Fasihi Simulizi katik Fasihi Andishi.tuliwajibika pia kutoa mifano kwengineko ili kubainisha kauli zetu.

Katika utangulizi wetu tulibainisha somo letu la utafiti pamoja na vigezo muhimu tulivyovitumi na methodolojia tulioitumia katika utafiti wetu.

Vilevile tulitalii kazi zingine za awali zilizowahi kutafitiwa na zenye uhusiano ulio wa karibu n utafiti wetu, ingawaje tulitumia nadharia tofauti kubainisha pengo lililokuwepo na ambal hatimaye tuliliziba. Pia tuliweza kufafanua malengo ya utafiti wetu katika sura hii.

Katika sura ya pili, tulishughulikia kwa kina tawasifu ya mwandishi Shaaban Robert na falsafa yake. Kutokana na tawasifu yake, tulibainisha kuwa, alikuwa ni mmoja wa waandishi wa kwanza wa kazi za nathari na vilevile alikuwa mshairi wa kutajika. Shaaban Robert kama tulivyoeleza inadaiwa kuwa ndiye mvumbuzi wa uandishi wa kinatharia na ni kiunzi kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi.

Tuliitathmini falsafa ya Shaaban Robert na kubainisha misingi yake katika sura hii ya pili. Aidha tulionyesha namna falsafa hii inavyojidhihirisha katika kazi zake za nadhari tukijikita katika riwaya yake *Utubora Mkulima*. Vilevile katika sura hii, tulichunguza namna asasi zingine za kijamii zilivyoathiri uandishi wa Shaaban Robert, hasa dini ya kiislamu iliyoletwa na wageni wa kwanza katika Upwa wa Afrika Mashariki. Katika utafiti wetu tulibainisha jinsi dini ya Kiislamu ilivyoathiri pakubwa mtazamo wa Shaaban Robert kuhusu maisha.

Tamanio la Shaaban Robert katika ujenzi wa jamii mpya, linaathiriwa na imani kuwa ukamilifu unaafikiwa akhera, na maisha ya sasa ni maandalizi tu ya maisha hayo ya akhera .Hili linamchora Shaaban Robert kama mhubiri katika uandishi wake.

Katika sura ya tatu utafiti wetu uliweka wazi shughuli nzima ya somo letu la utafiti. Katika kubainisha athari hizi, tuliangazia maana na umuhimu wa Fasihi Simulizi katika jamii. Aidha tuliuangazia mwingiliano matini katika utanzu wa Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi..

Utafiti wetu umedhihirisha kuwa Fasihi Andishi haipo bila Fasihi Simulizi, na waandishi wengi akiwemo Shaaban Robert wamechota, si wahusika, si mbinu, si maudhui kutoka kwa Fasihi Simulizi.

Kwa kujikita katika riwaya ya Shaaban Robert, ni bayana kuwa ameshughulikia maadili, haki, heshima, bidii, uhusiano na mengineyo katika jamii. Vivyo hivyo, Fasihi Simulizi ilisisitiza maadili yaya haya katika jamii. Hivyo basi Fasihi Andishi ni mwangwi wa Fasihi Simulizi.

Katika Fasihi Simulizi, wema walituzwa ilhali waovu waliadhibiwa. Shaaban Robert katika kuwasawiri wahusika wake, amejikita katika makundi mawili: ya wema na waovu. Wema wanafaulu katika maisha wakati ambapo waovu wanaangamia. Hii ni athari kutokana na Fasihi Simulizi.

Athari za Fasihi Simulizi katika uandishi wa Shaaban Robert, zi wazi na ithibati zake ni nyingi kama vile, usimulizi maizi ambao ni mbinu ya Fasihi Simulizi, matumizi ya tamathali za lugha zilizojikuta katika jamii yake ambazo zilikuwa kigezo muhimu katika busara ya fanani, wahusika, miisho ya hadithi, umuhimu wake katika jamii na kadhalika.

Katika sura ya nne, utafiti wetu umeshughulikia suala la usimulizi ambalo ni kitengo muhimu katika kufaulisha kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Utafiti wetu umeainisha aina za usimulizi kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kwa riwaya ya *Utubora Mkulima*. Aidha umuhimu wa kila aina ya usimulizi umebainishwa katika sura hii.

## 5.2 HITIMISHO

Utafiti wetu umebainisha ya kwamba ingawaje fasihi imaweza kugawanywa katika maeneo mawili makuu yaani Fasihi Andishi na Fasihi Simulizi, kwa hakika mgawanyiko huu una nyufa zinazotokana na ukweli kwamba Fasihi Andishi ina athari nyingi kutokana na Fasihi Simulizi kwa hivyo mgawanyiko huu haustahili kuchukuliwa kama mpaka ambao hauwezi kuvukwa.

## 5.3 MAPENDEKEZO

Tunapendekezea watafiti wa siku zijazo watafiti kuhusu maudhui katika riwaya hii ya *Utubora Mkulima.* Aghalabu wanaweza kuchunguza iwapo mawazo yake bado yanaweza kuifaa jamii ya kisasa.

Tungependekeza watafiti wa baada yetu watumie nadharia ya umuundo inayotokana na mawazo ya wanaisimu wa kiswisi, Ferdinand de Saussure na wenzake au nadharia nyingine mwafaka.

Vilevile tungeshauri watafiti wa baadaye wachunguze kipengele cha usimulizi kwa kina katika riwaya hii. Wanaweza kufanya hivyo kwa kutumia nadharia ya naratolojia.

Iwapo haya na mengineyo yatatekelezwa, bila shaka watachangia pakubwa katika ukuaji wa lugha na Fasihi ya Kiswahili na kuwanufaisha wasomaji wake.

# MAREJELEO


Gibbe A.G. (1980), *Mitaala ya Fasihi.*

Dar es Salaam. T.P.H

Madumulla J.S. (2009), *Riwaya ya Kiswahili. Nadharia na Misingi ya Uchambuzi.*

Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.

Mbatiah M. (2001), *Kamusi ya Fasihi.*

Nairobi: Standard Textbooks, Graphics and Publishing

Mbatiah M. (1990), *Mbinu za uandishi katika riwaya za mwazo za Shaaban Robert*

(Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi

Mulila A.K (2005), *Dhana ya mwingiliano matini*

(Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi

Msokile M. (1993), *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.*

Nairobi: E.A.E.P

Njogu K. na Chimerah R. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.*

Nairobi: JKF Publishers.

Njogu K. na R.M Wafula (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.*

Nairobi: K.L.B

Ogechi N. O et al (2008), *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.*

Eldoret: Moi University Press.

Senkoro F.E.M.K. (1982), *Fasihi.*

Dar es Salaam: Press and Publicity Center

Shaaban Robert (1968), *Utubora Mkulima.*

Nairobi: Evans Brothers

______________________(1936 na 1946), *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini.*

Nairobi: Evans Brothers.

Topan Farouk M. (1975), *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili.*

Dar es Salaam: Oxford University Press.

TUKI (1981), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.*

Dar es Salaam: Oxford.

Wamitila K.W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi Simulizi. Misingi na Vipengele Vyake.*

Nairobi Phoenix Publishers Ltd.

______________________ (2004), *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.*

Nairobi: Focus Publications Ltd.

Zaja J.O., (1986), *Fasihi tafsiri katika ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili, matatizo na athari zake*

(Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi